



ILANI YA UCHAGUZI MKUU WA RAIS, WABUNGE NA MADIWANI 2020 - 2025



UHURU, HAKI NA MAENDELEO YA WATU
CHAGUA CHADEMA
Oktoaba 28



Mheshimiwa Tundu A. M Lissu
Mgombea Urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



Mheshimiwa Salum M.J Mwalim

Mgombea Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania



YALIYOMO

1.0 UTANGULIZI	1
1.1 VIPAUMBELE VYA ILANI	5
2. MAMBO YA SIKU 100 ZA KWANZA	8
3. UONGOZI NA UTAWALA BORA.....	11
3.2 HAKI ZA BINADAMU	14
3.3 UTOAJI HAKI	15
3.4 UHURU WA KUJIELEZA.....	17
3.5 MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR	19
4. KUJENGA NA KUMILIKI UCHUMI IMARA NA SHIRIKISHI	21
4.1 SEKTA YA FEDHA	23
4.2 MFUMO WA KODI RAFIKI KWA WAVEKEZAJI NA WAFANYABIASHARA.	25
4.3 UCHUMI WA KIDIGITALI.....	29
5. ELIMU BORA KWA MAENDELEO ENDELEVU.....	32
5.1 MSONGAMANO WA WANAFUNZI	33
5.2 MASLAHI YA WALIMU	33
5.3 VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA	34
5.4 MFUMO WA ELIMU NA MITAALA	34
5.5 ELIMU YA JUU	35
5.6 UWEKEZAJI KATIKA LUGHA YA KUJIFUNZA NA KUFUNDISHIA.....	36
5.7 MPANGO WA MAENDELEO WA MIAKA 5 KATIKA ELIMU UMEFIFISHA SEKTA YA ELIMU.	37
6. AFYA, HIFADHI NA HUDUMA ZA JAMII.....	41
6.1 HIFADHI NA HUDUMA ZA JAMII	43
6.2 HUDUMA KWA WATU WENYE MAHITAJI MAALUM.....	44
6.3 MPANGO WA CHADEMA KUHUSU WANAWAKE NA WATOTO ...	45
6.4 FURSA ZA AJIRA NA UJIRA BORA KWA VIJANA.....	46



7. ARDHI, MAJI, MIPANGO MIJI, NYUMBA NA MAENDELEO VIJIJINI	49
7.2 FURSA YA KUPATA MAJI SAFI NA SALAMA KWA KILA MTANZANIA	53
8. KUJENGA KILIMO,UVUVI NA UFUGAJI	56
8.1 UVUVI WA BAHARI KUU (DEEP SEA FISHING)	62
9. MAZINGIRA, MABADILIKO YA TABIA NCHI NA NAMNA YA KUKABILIANA NA MAJANGA.....	66
9.1 MAZINGIRA.....	66
9.2 MABADILIKO YA TABIANCHI.....	66
9.3 KUKABILIANA NA MAJANGA.....	68
10.0 MIUNDOMBINU: UCHUKUZI, MAWASILIANO NA TEHAMA	70
10.2 UCHUKUZI: USAFIRI WA NCHI KAVU, USAFIRI WA MAJI, USAFIRI WA ANGA.	72
10.3 TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA).....	74
10.4 POSTA	75
11. MALI ASILIA NA UTALII.....	77
11.1 WANYAMAPORI	78
11.2 MISITU	79
11.3 UHIFADHI WA UOTO WA ASILI NA MAENEO ASILIA.....	80
11.4 UTALII	81
12. UZALISHAJI WA NISHATI NA MATUMIZI YA MADINI WENYE TIJA	84
12.1 Nishati.....	84
13. VIWANDA	87
14. MICHEZO, SANAA NA UTAMADUNI.....	89
15. ULINZI NA USALAMA.....	92
16. TANZANIA KATIKA DIPLOMASIA YA KIMATAIFA	95
16.1 KUKUZA NAFASI YA TANZANIA KATIKA DIPLOMASIA YA KIMATAIFA	95
16.2 IDARA YA UHAMIAJI	96

1.0 UTANGULIZI

MAENDELEO NA HAKI ZA WATU

Ilani ya Chadema ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani ya mwaka 2020 – 2025 imetungwa kwa kuzingatia misingi ya falsafa, itikadi pamoja na madhumuni ya kuanzishwa kwa Chadema, kama ilivyofafanuliwa kwa kina katika Sura ya 3 na Sura ya 4 ya Katiba ya Chadema (Toleo la 2019).

Kwanza, Ibara 3.1.3 ya Katiba ya Chadema inaitaja falsafa ya Chadema kuwa, “Ujenzi na udumishaji wa Demokrasia na Maendeleo nchini vitatokana na Nguvu na Mamlaka ya Umma wa Watanzania. Nguvu na Mamlaka ya Umma itabainishwa, kuainishwa na kulindwa katika Katiba ya Nchi; na Umma ndiyo utakuwa chimbuko la Katiba hiyo”.

Pili, Ibara ya 4.1.4 ya Katiba ya Chadema inatamka madhumuni ya Chadema kuwa ni: “Kuendeleza na kudumisha Demokrasia katika mfumo wa vyama vingi vya siasa, kujenga utamaduni wa demokrasia katika jamii kwa kutambua haki za wengi katika maamuzi; na pia kutambua haki za wachache kusikilizwa, kuheshimiwa na kulindwa, sambamba na kukubali ushindani huru, wa haki na wa wazi katika uchaguzi.”

Falsafa hii na madhumuni haya ya Chadema ni mwendelezo na maboresho ya falsafa na madhumuni yaliyoongoza juhudi za Watanzania kupigania uhuru wao toka kwa wakoloni. Juhudi hizi zilikuwa ni kiini cha ukombozi wa awamu ya kwanza wa Tanzania. Miaka kadhaa baada ya ukombozi wa awamu ya kwanza Watanzania wamejikuta wakihitaji ukombozi wa awamu ya pili. Ukombozi huu wa awamu ya pili unasukumwa na falasafa na madhumuni yanayofanana kwa vile, yanalenga kumtoa Mtanzania katika hali duni kwenda kwenye hali bora zaidi ya maisha.

Jambo hili limedhihirishwa na maono ya Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere yaliyoainishwa katika Ibara ya 28 ya Mwongozo wa TANU wa mwaka 1971, kwamba; *“Kwa watu ambao walikuwa watumwa, au ambao walikuwa wakionewa, wakinyonywa, na kunyanyaswa kwa sababu ya Ukoloni, Ukabaila au Ubepari, “Maendeleo” maana yake ni “Ukombozi”. Kitendo chochote kinachowapa uwezo zaidi wakuamua mambo yao wenyewe, ni kitendo cha maendeleo, japo kama hakiwaongezei afya wala shibe. Kitendo chochote kinachowapunguzia uwezo wao wa kuamua mambo yao wenyewe na kutawala maisha yao wenyewe, si kitendo cha maendeleo, ni kitendo cha kuwarudisha nyuma, japo kama kitendo chenyewe kinawaongezea afya na shibe kidogo.”*

Leo Tanzania inashuhudia, hususani katika Serikali ya Awamu ya Tano, vitendo vya watawala vinavyolenga kuwapunguzia wananchi *“uwezo wao wa kuamua mambo yao wenyewe na kutawala maisha yao wenyewe”* na hivyo kujikuta wakilazimika kuwa sehemu ya vuguvugu la ukombozi awamu ya pili. Katika vuguvugu hili, vyama vya siasa Tanzania vimejidhihirisha kuwa vya aina mbili: chama Dola cha CCM kinachotumia vyombo vya Dola kulazimisha kubaki madarakani na kuendelea kuongoza Dola kwa upande mmoja; na vyama vya upinzani halisi ambavyo agenda yake kuu ni kukipumzisha chama Dola ili kikome kuendelea kuongoza Dola na kutokomeza ushawishi wa hoja kuwa, maendeleo yanahitaji kuwepo Mtawala wa kimila badala ya kushamiri kwa ushindani wa mawazo mbadala.

Leo Tanzania ipo kwenye zama za kudai katiba mpya inayopanua wigo wa utawala wa kidemokrasia na Serikali ya “Jamhuri” kamili yenye kutokomeza Urais wa kifalme na kisultani ambapo Rais anateua mlolongo wa viongozi tangu Wilaya hadi Taifa. Leo wananchi wako katika vuguvugu la harakati ya kuhakikisha utawala wa sheria unalindwa kikweli kweli kwa kutenganisha mamlaka za mihimili ya Serikali, Mahakama na Bunge, ili kila mhimili ufanye kazi zake kwa uhuru mpana na wa kina bila

kuingiliwa na mhimili mwingine. Leo wananchi ni sehemu ya vuguvugu la kudai uwajibikaji kwa umma na uadilifu mpana na wa kina wa watendaji wote wa vyombo vyote vya maamuzi na utendaji.

Kwa mantiki hii, bila demokrasia ya kweli haiwezekani kuwepo maendeleo ambayo ni ukombozi! Maendeleo ya aina hii huwafanya wanaonufaika nayo wawe watu wanaojisikia kuwa utu wao na ubinadamu wao haujabezwa au kudhalilishwa katika kuyapata maendeleo yale kama vile kuaminishwa kuwa maendeleo yanatolewa kwa watu kama fadhila ya Mkuu wa Nchi.

Maendeleo ambayo ni ukombozi yanatokana na juhudi za wale wanaonufaika nayo kama vile kutokana na wao kulipa kodi au kutokana na jasho lao au msaada kutoka kwa ndugu au rafiki anayeguswa na juhudi za mhusika kusaka maendeleo yake na kuwiwa kutaka kuunga mkono juhudi hizo. Ila misaada ya aina hii lazima iwe imetokana na mtoaji msaada kufanya hivyo kama ishara ya kuwa katika mshikamano na watu walio kwenye juhudi za kujiletea maendeleo na si hisani inayotolewa ikiambatana na dharau na kebehi!

Ni wazi sasa kuwa, leo chama tawala Tanzania ni mfumo ambao kuuondoa lazima kuunganisha nguvu za wote (wanachama wa Chadema na wasio wanachama wa Chadema) wenye kuwa na sababu ya kuung'oa mfumo huu wa ulevi wa madaraka unaotokana na KATIBA ya 1977. Katiba hiyo kwa mfano inaruhusu kuwepo Urais wa kisultani wenye kuwa na mamlaka ya kuteua watendaji wa karibu ngazi zote na wa mihimili yote ya Dola bila kuhojiwa na yeyote kiasi cha kufikia hata kila tamko la Rais kuchukuliwa kuwa ni '*sheria*' hata kama amri hiyo inakiuka Katiba na Sheria za Nchi.

Lengo kuu la ujumla la Ilani hii, ni kukuhamasisha wewe Mtanzania mpiga kura, kuwa na kila sababu ya kuchagua wagombea wa Chadema. Ilani imebeba falsafa, madhumuni, na

sera za Chadema kuhusiana na masuala mbalimbali yanayogusa maisha ya kila siku ya Mtanzania hususani ya uongozi, utawala na uchumi; ikiwa ni pamoja na kilimo, uvuvi, ufugaji, viwanda na huduma za biashara; huduma za jamii kama elimu, afya na maji, mipango miji na maendeleo vijijini; nishati, mali asili; utalii, utamaduni, michezo na vijana, ajira na ujasiriamali; afya na ustawi, wazee; wanawake na watoto; ulinzi na usalama; na diplomasia ya kimataifa.

Ilani inaonesha kwa kifupi mahali tulipo kama Taifa na wapi tunataka kwenda kama Watanzania wanaojitambua kuwa Desemba, 2020 tutatimiza miaka 59 ya uhuru wa bendera na ukombozi awamu ya kwanza kwa kupata uhuru toka kwa Mkoloni.

Ilani hii inalenga kuwapa matumaini wapiga kura, wale wanaojitambua na wameshuhudia jinsi Serikali ya CCM iliyopo mdarakani ilivyopanga vipaumbele vya kisera na utekelezaji wake kwa njia za kibabe na kinyapara, bila kushirikisha kikamilifu taasisi za uwakilishi kama Bunge na Halmashauri, kuwa yote haya yatakoma pale wakiichagua serikali ya Chadema ambayo inawapa ahadi thabiti kuwa itarekebisha namna nchi inavyoongozwa kwa:

- a) Kudumisha amani, umoja na mshikamano wa taifa, yote yakiwa zao la kuwa na Katiba na sheria zinazosimamia haki na usawa kwa wananchi wote.
- b) Kuujenga na kuuimarisha Muungano wa Shirikisho kati ya nchi washirika za Zanzibar na Tangayika kuzaa Tanzania kwa kuzingatia misingi ya usawa na umoja unaoheshimu tofauti za msingi kati ya nchi zilizo kwenye Muungano.
- c) Kuwajengea mazingira wezeshi na kuyapa kipaumbele maswala yanayogusa maisha ya watu wa makundi yenye mahitaji maalum kama wanawake, watoto, vijana, wazee, na wanaoishi na ulemavu.

- d) Kuhimiza maridhiano, kujenga muafaka wa kitaifa na kushirikishana katika kutoa maamuzi.
- e) Kujenga Uchumi shirikishi wenye kulenga maendeleo ya watu; na kama maendeleo ya vitu basi yawe yale yenye kuimarisha uwezo wa wananchi walio wengi kujiletea maendeleo wenyewe bila kufanywa watumwa wa vitu au watwana wa watu wengine.
- f) Kujenga ushirikiano wa karibu baina ya Serikali na Sekta Binafsi kwa lengo la kuhimiza utekelezaji wa sheria na kanuni za ushirikiano huo kama vile kuhusu ulipaji kodi wa hiari na mapenzi ya kujenga taifa pamoja na kutekeleza mikataba ya ajira yenye kuzingatia maslahi stahiki ya waajiriwa na waajiri.
- g) Kuhimiza utekelezaji wa majukumu ya vyombo vya dola wenye kuongozwa na haki za binadamu zilizoainishwa kikatiba na kisheria pamoja hekima kwa kuzingatia dhana ya dola linalotumikia watu badala ya watu kutumikia dola.
- h) Kudumisha na kuendeleza uhuru wa mawazo, uhuru wa kutoa na kupata habari na kujumuika na wengine kama nyenzo ya kutoa nafasi kwa ubunifu kushamiri ambao ni nyenzo ya kuboresha elimu na na hatimaye ukuaji wa uchumi kwa ujumla.
- i) Kuimarisha huduma za jamii ikiwa ni pamoja na elimu bora kwa wote, afya njema kwa wote, maji safi na salama kwa wote, makazi bora kwa wote; na utayari wa kukabili majanga pamoja na magonjwa ya mlipuko kwa umakini.

1.1 VIPAUMBELE VYA ILANI

Ilani hii inaainisha maeneo yatakayopewa kipaumbele na serikali ya Chadema, vipaumbele hivyo ni pamoja na:

- a. Kugatua madaraka ya uongozi na utawala kwa lengo la kuusogeza karibu na wananchi

- b. Kubadili mfumo wa uongozi na utawala ili kuongeza na kuzingatia misingi ya uadilifu, ufanisi, uzalendo na uwajibikaji
- c. Kwa kushirikiana na sekta binafsi Kujenga uchumi imara wa kidigitali na shirikishi
- d. Kuongeza mishahara na kuwapandisha madaraja watumishi wa umma
- e. Kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa ndani na nje
- f. Kurejesha mchakato wa Katiba Mpya kuanzia ilipoishia Rasimu ya Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Jaji Warioba
- g. Kurejesha uhuru wa vyombo vya habari na uhuru wa kujieleza na kutoa maoni
- h. Kutoa elimu bora na bure kwa ngazi zote
- i. Kuanzisha utaratibu wa afya bure kwa akinamama wajawazito, watu wenye ulemavu, watoto na wazee
- j. Kuwajengea uwezo wanawake kusimamia na kumiliki uchumi
- k. Kwa kushirikiana na sekta binafsi kuongeza wigo wa ajira na kipato chenye tija kwa vijana
- l. Kwa kushirikiana na sekta binafsi ili kuhakikisha upatikanaji wa maji safi, salama na ya uhakika kwa wote.
- m. Kuwezesha Wananchi kumiliki ardhi kwa matumizi endelevu
- n. Kushirikiana na sekta binafsi kuboresha miundombinu ya barabara, masoko, nishati na viwanda vya kusindika mazao vijijini.
- o. Kutumia rasilimali ya maji iliyopo kwa ajili ya kilimo cha umwagiliaji na mifugo.

- p. Kushirikiana na sekta binafsi Kuboresha miundombinu ya barabara, reli, usafiri wa anga na majini.
- q. Kushirikiana na sekta binafsi kuboresha sekta ya utalii na maliasili.
- r. Kushirikiana na sekta binafsi kuhakikisha uwepo wa Nishati nafuu na ya uhakika.
- s. Kuboresha sekta ya madini na kuwezesha wachimbaji wadogo wanashiriki na kumiliki uchumi wa madini.
- t. Kushirikisha sekta binafsi katika kuimarisha sekta ya sanaa, utamaduni na michezo na kuifanya iwe ya kibiashara.

Ilani hailengi kusheheni ahadi hewa bali dira ya kile serikali ya Chadema itakachotekeleza baada ya kupata ridhaa kufutilia mbali madhara ya kuwepo kwa dola lililoongozwa na chama dola kilichojiona kuwa juu ya matakwa ya wananchi. Ilani hii imebeba maono na mwelekeo wa kisera wa Serikali ya Chadema kwa lengo la kuwashawishi wapiga kura kuchangua wagombea wa Chadema kwa vile Chadema kinaamini katika “UHURU, HAKI NA MAENDELEO YA WATU”

2. MAMBO YA SIKU 100 ZA KWANZA

Ndani ya siku 100 tangu siku ya kuapishwa kwa Rais na Wabunge, watakaokuwa wamechaguliwa, Serikali ya Chadema itafanya taratibu zinazohusika ili kuhakikisha yafuatayo yanatendeka:

- i) Serikali itapeleka Bungeni Muswada wa Sheria ya Maridhiano, ambayo pamoja na mambo mengine itaanzisha Tume ya Maridhiano kwa lengo la kuondoa hofu ya uwezekano wa vitendo vya kulipiza visasi na kuunganisha nguvu za wananchi wote bila ubaguzi wa vyama katika kuongoza Taifa letu.
- ii) Serikali itapeleka Bungeni Muswada wa Sheria ya Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi juu ya Utoaji wa Elimu Bure kuanzia elimu ya awali hadi Sekondari.
- iii) Serikali itapunguza kiwango cha marejesho ya mikopo ya elimu ya juu hadi kufikia asilimia tatu (3) ya mshahara wa mnufaika na kutanua wigo wa muda wa marejesho hadi kufikia miaka 25 tangu mnufaika apate ajira. Aidha, Serikali itafuta riba na tozo zote zitokanazo na adhabu ya kuchelewesha marejesho ya mkopo wa elimu ya juu.
- iv) Serikali itashirikiana na sekta binafsi kuweka utaratibu wa kutoa huduma za afya ya msingi kwa wananchi bila malipo.
- v) Serikali itarejesha mchakato wa Katiba Mpya kuanzia ilipoishia Rasimu ya Tume ya Marekebisho ya Katiba ya Jaji Warioba
- vi) Serikali ya Chadema itatekeleza matakwa ya Katiba kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano ili kila nchi Mshirika wa Muungano ipate mgao wake wa fedha kwa mujibu wa Katiba na sheria.
- vii) Serikali ya Chadema itarejesha uhuru wa vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na kuruhusu vyombo hivyo kurusha moja

- kwa moja vikao vya Kamati za Bunge, Mikutano ya Bunge na Mwenendo wa Uendeshaji wa Mashauri Mahakamani.
- viii) Serikali ya Chadema itapeleka miswada ya Sheria Bungeni kwa madhumuni ya kuzifuta Sheria zote kandamizi na zinazokiuka misingi ya haki za binadamu.
 - ix) Kuanzisha utaratibu wa mazungumzo kati ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar kwa lengo la kufikia muafaka juu ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi, uvuvi wa bahari kuu na usajili wa meli.
 - x) Serikali ya Chadema itaandaa mazingira rafiki na wezeshi kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari walioshindwa kuendelea na masomo kwa sababu mbalimbali kama vile ugonjwa, kukosa ada, mimba n.k. kurejea kwenye mfumo rasmi wa elimu na kumalizia masomo yao.
 - xi) Serikali ya Chadema itapeleka bajeti ya Nyongeza Bungeni katika mwaka wa fedha 2020/2021 kwa ajili ya kuongeza Mishahara ya watumishi wote wa umma, kulipa malimbikizo; sambamba na kuwapandisha madaraja watumishi wenye sifa na kulipa mishahara inayoendana na madaraja yao.
 - xii) Serikali ya Chadema itaanzisha bima maalum ya afya kwa watumishi wote wa vyombo vya Ulinzi na Usalama wawapo kazini na baada ya kustaafu vikiwemo Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zima moto na Uokoaji.
 - xiii) Serikali ya Chadema itarejesha maduka yasiyotozwa kodi (Duty free shops) katika vyombo vya ulinzi na usalama vikiwemo Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Polisi, Magereza, Uhamiaji, Zimamoto na Uokoaji.
 - xiv) Serikali itapeleka Bungeni Muswada wa Marekebisho ya Sheria ya Hifadhi ya Jamii ili kurekebisha kikokotoo cha

Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa wastaafu ili kiendane na mahitaji ya wastaafu. Aidha, Serikali ya Chadema itaruhusu wafanyakazi na watumishi waliochangia katika mifuko ya jamii kuchukua mafao yao wakati wowote (fao la kujitoa).

- xv) Serikali ya Chadema itaweka utaratibu na kuwatafutia masoko wakulima, wavuvi na wafugaji ya kuuza mazao yao ndani na nje ya nchi bila kizuizi.
- xvi) Kurejesha utaratibu wa awali wa ukusanyaji wa kodi, ushuru na tozo mbalimbali kwa mamlaka ya serikali za mitaa

3. UONGOZI NA UTAWALA BORA

Uongozi unaozingatia misingi ya utawala bora, utawala wa sheria na uwajibikaji wa viongozi na watumishi wa umma ni hitaji la msingi la Serikali inayowajibika kwa wananchi. Chadema inaamini katika utawala bora utakaozingatia uwazi na uwajibikaji Serikalini na wananchi kushirikishwa katika kuamua masuala muhimu yanayohusu maisha yao.

Kwa kuwa kumekuwa na ukiukwaji mkubwa wa misingi ya kidemokrasia, utawala bora, utawala wa sheria, na uwajibikaji duni wa viongozi na watumishi wa umma katika muhula wa uongozi uliopita; Serikali ya Chadema inakusudia kufanya mambo yafuatayo katika eneo la Utawala Bora:-

- a. Kuwashirikisha wananchi kutoa maoni na mapendekezo katika mchakato wa kutunga sheria zote za nchi ili kurahisisha usimamizi na utekelezaji wa sheria hizo.
- b. Kuhakikisha kuwa demokrasia inakuzwa kwa kuanzisha Tume Huru ya Uchaguzi ili kupata viongozi bora waliochaguliwa kidemokrasia.
- c. Kuhakikisha kuwa Wananchi wanakuwa na nguvu ya kuwawajibisha viongozi wao katika ngazi mbalimbali kupitia michakato mbalimbali kwa mujibu wa sheria na taratibu zitakazowekwa.
- d. Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa kuna uwazi katika utendaji wa Serikali. Kwa sababu hiyo, mikataba yote ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya kiuchumi na uwekezaji itapelekwa Bungeni kwa ajili ya kupata idhini ya Bunge kabla Serikali haijaingia katika mikataba hiyo.
- e. Serikali ya Chadema itarejesha uhuru wa vyombo vya habari ikiwa ni pamoja na kuruhusu vyombo hivyo kurusha moja kwa moja vikao vya Kamati za Bunge, Mikutano ya Bunge na Mwenendo wa Uendeshaji wa Mashauri Mahakamani.

- f. Serikali ya Chadema itapeleka miswada ya Sheria Bungeni kwa madhumuni ya kuzifuta Sheria zote kandamizi na zinazokiuka misingi ya demokrasia, haki za binadamu na utawala bora.
- g. Serikali ya Chadema itadumisha dhana ya mgawanyo wa madaraka katika mihimili ya Dola (Serikali, Bunge na Mahakama) kwa kuondoa vikwazo vya kiutawala na kibajeti vilivyokuwa vinasababisha mwingiliano wa majukumu miongoni mwa mihimili hiyo; na hivyo kuathiri utendaji wake wa kazi.

3.1 UGATUAJI WA MADARAKA

Ugatuaji wa madaraka ni mfumo wa Serikali ambapo mamlaka ya Dola inatokana na wananchi, kupitia Serikali za shirikisho zilizochaguliwa, huku masuala ya jumla ya kitaifa yakibaki chini ya Serikali Kuu.

Mfumo wa utawala wa nchi yetu kwa sasa unaipa mamlaka makubwa Serikali Kuu kuliko Serikali za Mitaa ambazo zimeanzishwa kwa mujibu wa ibara ya 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na Sheria namba 7 na 8 za mwaka 1982.

Hali ilivyo sasa ni kwamba, Serikali Kuu imezipoka Serikali za Mitaa mamlaka ya kujitegemea na kujiendesha. Mathalani, Serikali Kuu imechukua vyanzo vingi vya mapato vya Serikali za Mitaa na kuviweka chini ya mamlaka ya Serikali Kuu jambo ambalo limezifanya Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji kushindwa kujitegemea na kujiendesha na hivyo kubaki tegemezi kwa Serikali Kuu. Vyanzo hivyo vya Mapato ni kama vile kodi ya majengo, kodi ya mabango na ushuru wa biashara kwa wajasiriamali wadogo.

Shughuli zilizokuwa zinasimamiwa na Serikali za Mitaa moja kwa moja kama vile ujenzi wa miundombinu ya barabara nazo

zimeanza kusimamiwa na Serikali Kuu kupitia Mawakala wa Serikali Kuu. Kwa mfano, Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA) haziwajibiki kwenye Mabaraza ya Madiwani ya Halmashauri husika jambo ambalo kwa dhahiri limepoka mamlaka ya mabaraza hayo katika kusimamia miradi ya maendeleo katika maeneo yao. Aidha, Serikali Kuu imejipa mamlaka makubwa kwenye usimamizi wa Shule za Msingi na Sekondari pamoja na Zahanati na Vituo vya Afya ambapo kazi hiyo ingefanywa kwa ufanisi zaidi na Serikali za Mitaa, huku Serikali Kuu ikibaki na mamlaka ya kutunga Sera na Miongozo mbalimbali ya utekelezaji wa Sera hizo .

Kwa kuwa, Falsafa ya Chadema imejikita kwenye **“Nguvu na Mamlaka ya Umma”** katika kuongoza Nchi, hivyo basi, **Serikali ya Chadema itafanya mambo yafuatayo:-**

- a. Itapeleka madaraka kamili kwa wananchi kupitia Serikali za Majimbo na Mitaa, na kufuta sheria zote zinazopoka madaraka katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.
- b. Itaziimarisha Serikali za Majimbo na Mitaa kwa kuhakikisha kuwa zinakuwa huru katika kubuni, kukusanya na kutumia mapato yatokanayo na vyanzo vya ndani
- c. Itahakikisha kwamba, Serikali za Majimbo na Mitaa zinatoa huduma za jamii kama vile elimu, afya na maji na kwamba huduma hizo zitakuwa karibu na kumilikiwa na wananchi.
- d. Itahakikisha kuwa viongozi wote katika mfumo wa Serikali za Majimbo na Mitaa wanachaguliwa na wananchi.
- e. Itahakikisha kwamba kila Halmashauri inatenga bajeti kwa ajili ya kikosi cha zimamoto na uokoaji ili kuhakikisha kwamba kikosi hicho kinakua na ufanisi kukabiliana na majanga pindi yanapotokea.

3.2 HAKI ZA BINADAMU

Haki za Binadamu ni haki anazostahili kuwa nazo kila mtu kutokana na yeye kuwa binadamu. Haki hizi ni za kuzaliwa, na hazitolewi na mtu yeyote au chombo chochote kama fadhila, bali ni lazima kila mtu afurahie haki hizo kwa kuwa yeye ni binadamu. Haki hizo ni pamoja na haki ya kuishi, haki ya kutendewa kama binadamu bila kutwezwa utu wa mtu na haki ya kulindwa na kuwa mtu huru.

Kwa bahati mbaya kumekuwa na ongezeko la ukiukwaji wa haki za binadamu hapa nchini kwa miaka mitano iliyopita, jambo ambalo limezua taharuki miongoni mwa wananchi na hivyo kujihisi kuwa hawako salama katika nchi yao. Kwa mfano imeshuhudia kuongezeka kwa vitendo mbalimbali vya mauaji, utekaji na utesaji vikidaiwa kufanywa na **“Watu wasiojulikana”**.

Watu mbalimbali wakiwemo wanahabari, wasanii, wanasiasa wa upinzani na wa Chama Cha Mapinduzi walitekwa, kuteswa, kupigwa risasi na wengine hawajawahi kupatikana mpaka leo. Aidha, matukio hayo yalienda sambamba na kuzagaa kwa miili ya watu waliouwawa kandokando ya mito mbalimbali na katika fukwe za Bahari ya Hindi. Aidha, Tumeshuhudia kutumika kwa sheria ya makosa ya mtandao kama sehemu ya kuwanyamazisha, kuwaweka mahabusu na kuwafunga baadhi ya wanasiasa na wanaharakati wa haki za binadamu waliokuwa wanatekeleza wajibu wao kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Nchi.

Sheria za utakatishaji fedha (The Anti-Money Laundering Act) na sheria ya uhujumu uchumi (The Economic and Organised Crime Control Act) pia zimetumika kama njia ya kuwanyima dhamana watuhumiwa wengi wa makosa hayo kinyume kabisa na misingi ya haki kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo imeridhiwa na nchi yetu. Jambo hilo limesababisha watu mbalimbali kukaa mahabusu kwa muda mrefu bila

kusikilizwa kwa kisingizio cha upelelezi kutokamilika na au kusubiri ushahidi kutoka nje.

Kwa kuwa, Chadema inaamini na inasimamia haki za Binadamu, ambazo kila mtu anastahili kuwa nazo kama zilivyoainishwa katika Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu na Mikataba ya Kimataifa juu ya usimamizi wa haki hizo; Serikali ya Chadema itafanya mambo yafuatayo kwenye eneo la Haki za Binadamu:-

- a. Kutekeleza mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu itakayoridhiwa na Bunge na kufuta sheria zote za ndani zinazokandamiza haki za Binadamu.
- b. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba, uhai wa kila mtu unathaminiwa na unalindwa.
- c. Serikali ya Chadema itaunda Tume ya Maridhiano ya kitaifa kwa ajili ya kuliunganisha Taifa kutokana na uwepo wa matukio ambayo yamejenga chuki, hasira na uhasama miongoni mwa wananchi na vyombo vya dola, na hivyo kuliunganisha taifa kuwa kitu kimoja.
- d. Serikali ya Chadema itaunda Tume ya Majaji wa Mahakama (Judicial Commission of Inquiry) kwa ajili ya kuchunguza vifo na matukio yote ya ukiukwaji wa haki za binadamu yenye utata yaliyotokea ndani ya miaka mitano iliyopita.
- e. Serikali ya Chadema itaifanyia marekebisho ya kimfumo na kiutendaji Tume ya Haki za Binadamu na Utawala bora ili itekeleze majukumu yake bila kuingiliwa na Serikali kwa ajili ya kusimamia na kutoa taarifa kuhusu haki za binadamu nchini.

3.3 UTOAJI HAKI

Kwa mujibu wa Ibara ya 107A ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mahakama ndio mhimili wa dola wenye kauli ya mwisho kuhusu utoaji haki nchini.

Hata hivyo, pamoja na mamlaka hayo ya kikatiba, Mahakama imekuwa ikikabiliwa na changamoto mbalimbali ikiwa ni pamoja na amri za Mahakama kutotekelezwa kikamilifu na mhimili wa Serikali; Mahakama kukosa uhuru kamili hasa kwenye kuajiri watumishi wake yenyewe, na pia kuwa tegemezi kwa mhimili wa Serikali kuhusu rasilimali fedha. Aidha, kumekuwa na changamoto ya ukosefu wa chombo kimoja cha uratibu wa mahakama na Magereza, na hivyo kuleta msuguanu kati ya mahakama na magereza hususani pale magereza inaposhindwa kutekeleza amri za Mahakama. Changamoto hizi, zimepelekea matatizo ya mlundikano wa mashauri mahakamani, ucheleweshaji wa kutoa maamuzi ya mashauri na miundombinu mibovu ya mahakama.

Kwa kuwa Chadema inapigania haki, usawa na ushirikishwaji wa jamii pamoja na mifumo huru ya sheria na utoaji haki; na kwa kuwa Chadema inatambua kwamba watu wote ni sawa mbele ya sheria; na kwa kuwa Chadema inapenda kila mtu atendewe haki; na kwa kuwa Chadema inakusudia kujenga jamii yenye uadilifu na tabia njema ambapo vitendo vya kihalifu vinapunguzwa au kutokomezwa; hivyo basi, Serikali ya Chadema itafanya mambo yafuatayo katika eneo la Utoaji haki:-

- a. Itawachukulia na kuwahesabu watuhumiwa wote kama watu wenye haki hadi hapo mahakama itakapowatia hatiani.
- b. Itahakikisha kwamba mhimili wa mahakama unakuwa huru na kwamba hauingiliwi na mtu, chombo au taasisi yoyote katika kutoa uamuzi wake ili kuhakikisha kwamba, haki inatolewa bila upendeleo wowote.
- c. Itahakikisha kuwa, Magereza yote yanatumika kama vituo vya kurekebisha tabia na kujenga mahusiano mapya badala ya kuwa sehemu za kuadhibu na kutesa wananchi.
- d. Itaunda Wizara moja itakayoshughulikia masuala ya utoaji haki kuliko ilivyo sasa ambapo masuala hayo

yanashughulikiwa na wizara zaidi ya moja ili kupunguza uwasimu katika uamuzi wa mashauri mahakamani na utekelezaji wa amri za mahakama.

- e. Itahakikisha kwamba Mahakama inajitegemea kwa rasilimali fedha na pia inakuwa na malaka kamili katika kuajiri watumishi wake yenyewe kupitia Tume ya Utumishi ya Mahakama bila kuomba kibali katika mhimili wa Serikali.
- f. Ili kupunguza mrundikano wa mahabusu katika Magereza nchini, Serikali ya Chadema itafanya marejeo ya sheria mbalimbali ili makosa yote yenye kustahili dhamana yapewe dhamana kwa mujibu wa sheria.
- g. Itahakikisha kwamba kunakuwa na mfumo wa kuchukua kumbukumbu (hansard) za mwenendo wa mashauri kuanzia mahakama za wilaya mpaka mahakama kuu na divisheni zake zote, ili kuharakisha utolewaji wa mapema wa uamuzi wa mashauri mahakamani kuliko ilivyo sasa ambapo ni Divisheni ya Biashara pekee ndiyo inayotumia utaratibu huo.
- h. Itaruhusu vyombo vya habari kurusha moja kwa moja mwenendo wa mashauri mahakamani.
- i. Kwa ajili ya kudumisha uwajibikaji na utawala bora; majaji wote wa Mahakama Kuu wataomba ajira hiyo kwa Tume ya Utumishi ya Mahakama; na watakaokidhi vigezo watathibitishwa na Bunge.

3.4 UHURU WA KUJIELEZA

Uhuru wa kujieleza unajumuisha uhuru wa kukusanyika, kujieleza, kuchora, haki sawa ya kutumia vyombo vya habari vya umma, kutafuta na kusambaza habari pamoja na kuwa na faragha. Pamoja na ukweli kwamba Ibara ya 18 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetoa haki na uhuru kwa kila mwananchi kupata na kusambaza habari na kuwa huru

kueleza fikra zake; lakini haki na uhuru huo vimekanyagwa sana na watawala.

Kama Taifa, tumeshuhudia matangazo ya moja kwa moja ya mijadala ya Bunge yakifutwa na hivyo kuwanyima wananchi haki ya kupata habari juu ya mijadala ya wawakilishi wao Bungeni, tumeshuhudia magazeti yanayoandika habari za kiuchunguzi na kukosoa utendaji wa Serikali yakifungwa na mengine kufutwa kabisa, tumeshuhudia baadhi ya vituo vya redio vikipewa adhabu ya kufungwa kutokana na kurusha habari zinazohusu utendaji wa Serikali na pia tumeshuhudia waandishi wa habari wakikamatwa na kufunguliwa keshi za uhujumu uchumi na wengine kutekwa na kuuwawa. Aidha, tumeshuhudia utungwaji wa sheria ngumu na kandamizi za Makosa ya Kimtandao, Sheria ya Takwimu, na Sheria ya Huduma za Vyombo vya Habari, zote zikilenga kuminya uhuru wa kupata na kusambaza habari.

Kwa kuwa Chadema inaamini katika fikra huru na mawazo mbadala kama msingi wa ujenzi wa uchumi shirikishi na hivyo kuleta maendeleo endelevu katika taifa; hivyo basi, Serikali ya Chadema itafanya mambo yafuatayo katika eneo la uhuru wa kujieleza:-

- a. Itahakikisha kwamba kila mwananchi anakuwa na uhuru kamili wa kueleza fikra zake, kupata na kutoa habari, kukusanyika na kujiunga na kikundi au chama chochote kwa hiari na utashi wake.
- b. Itahakikisha kwamba, vyombo vyote vya habari; vya umma na binafsi, vinakuwa na uhuru wa kutafuta na kutoa habari bila upendeleo.
- c. Itahakikisha kwamba, sheria zote zinazokandamiza uhuru wa habari zinafutwa; na kila mwananchi atakuwa na haki na fursa sawa ya kutumia vyombo vya habari vya umma.
- d. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba inachunguza matukio ya vifo na utekaji wa waandishi wa habari

waliokumbwa na mikasa hiyo wakati wa utekelezaji wa majukumu yao.

3.5 MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR

Suala la Muungano ni agenda muhimu kwa mustakabali wa mshikamano na umoja wa kitaifa. Hata hivyo, Muungano huo umekuwa ukilalamikiwa kutokana na muundo wake kutokidhi makusudio yaliyotarajiwa. Matalani, yapo maoni kuwa Zanzibar, ambayo ni nchi mshirika wa Muungano hainufaiki vya kutosha kutokana na aina ya muungano uliopo jambo, ambalo lilisababisha kuwepo kwa kero za Muungano, ambazo kwa muda mrefu zimekuwa zikishughulikiwa bila kupata suluhisho la kudumu. Aidha, kumekuwa na malalamiko kwamba, Muundo wa Muungano wa Serikali Mbili uliopo sasa haukutokana na maoni na mapandekezo ya wananchi.

Kwa kuwa Chadema inaamini katika Muungano wenye maridhiano na unatokana na maoni na mapendekezo ya wananchi kwa mustakabali wa umoja na mshikamano wa Taifa letu; Serikali ya Chadema itafanya yafuatayo katika eneo la Muungano:-

- a. Kupitia mchakato wa Katiba Mpya, Serikali ya Chadema itabadili Muundo wa Muungano kutoka mfumo wa Serikali mbili kwenda kwenye mfumo wa Serikali tatu; ambapo kutakuwa na Serikali ya Shirikisho la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Serikali ya Tanganyika na Serikali yenye mamlaka kamili ya Zanzibar.
- b. Kila nchi mshirika wa Muungano itakuwa na mamlaka kamili katika kumiliki na kutumia rasilimali na maliasili zake; isipokuwa masuala yote yanayohusu Muungano, yataamuliwa kwa maridhiano kati ya Serikali za nchi washirika.
- c. Serikali ya Chadema itaanzisha utaratibu wa mazungumzo kati ya serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar yenye lengo la kufikia muafaka kuhusiana na

- uendeshaji wa uchumi, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi, uvuvi wa bahari kuu, na usajili wa meli za kimataifa.
- d. Serikali ya Chadema itatekeleza matakwa ya Katiba kuhusu Tume ya Pamoja ya Fedha ya Muungano kama ilivyoainishwa katika Katiba ya sasa ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ili kuhakikisha kuwa Zanzibar inapata mgawo wake wa fedha wa mujibu wa Katiba.
 - e. Serikali ya Chadema itaanzisha mchakato wa kuanzisha na kuunda Mahakama ya pamoja ya usuluhishi wa migogoro ya Kikatiba ya Jamhuri ya Muungano.
 - f. Serikali ya Chadema itaanzisha mchakato wa Zanzibar kurejesha hadhi na mamlaka yake ya kujiunga katika vyombo vya kimataifa na kikanda.

4. KUJENGA NA KUMILIKI UCHUMI IMARA NA SHIRIKISHI

Uchumi ni nyanja kuu katika maendeleo ya binadamu. Kwa kutambua hilo Chadema kimejipanga kuutafsiri ukuaji wa uchumi kwa vitendo ili kuwepo kwa mabadiliko chanya katika maisha ya kila Mtanzania. Hili litawezekana kwa kufumua mfumo wa sasa wa uchumi wa kijamaa ambao umeshindwa kuboresha hali ya maisha ya Watanzania, na kuanzisha mfumo wa soko jamii ambao unalenga kufungua fursa kwa kila mtu kutumia vipaji vyake katika kuzalisha na kumiliki mali. Mfumo huu mpya wa uchumi wa soko utaambatana na uanzishaji wa uchumi wa kidigitali ambao unazidi kushika kasi katika nyanja zote za uzalishaji na utoaji huduma katika dunia ya utandawazi.

CHADEMA itafanya yafuatayo ili kujenga na kuimarisha uchumi;

Ilikuwa na uchumi jumuishi na shirikishi serikali ya Chadema imejiandaa kukuza na kuimarisha uchumi wa nchi kwa kutumia rasilimali za nchi yetu bila kuathiri uhuru wa Taifa, na kuhakikisha kuwa umma unanufaika na rasilimali zao kwa kufanya yafuatayo;

- a. Kujenga, kuimarisha na kusimamia uchumi wa kitanzania kwa kuwawezesha Watanzania kuwekeza kwa njia ya ubia na hisa na wawekezaji wenye mitaji mikubwa.
- b. Kuimarisha uchumi wa soko huru, utakaoheshimu na kulinda haki na mali za watu, biashara huru na sekta binafsi bila kupoka mamlaka ya umma katika maeneo nyeti.
- c. Kuimarisha mfumo wa kodi nchini ili kuwa na mfumo wa ulipaji kodi unaoendana na kipato cha mtu badala ya mfumo wa sasa ambao sio rafiki na unawaacha watu wengi bila kulipa kodi.
- d. Kufuta baadhi ya misamaha ya kodi kwenye baadhi ya maeneo na kuweka misamaha ya kodi maeneo nyeti tu na

- hasa yanayochochea ukuaji wa uchumi
- e. Kutoa mishahara inayoendana na uhalisia wa hali ya maisha kwa watumishi wote wa umma kuendana na ujuzi, nafasi, na vyeo vyao kazini
 - f. Kupanua wigo wa mapato yatokanayo na kodi, ili kuipatia serikali mapato ya kutosha.
 - g. Kuchochea ukuaji wa kilimo cha kitaalamu na kibiashara kwa kuyaongezea mazao thamani ili kitumike kama daraja la kuingia kwenye uchumi wa viwanda vyenye kusaidia kuwepo kwa mnyororo wa thamani wa mazao ya kilimo.
 - h. Kuwawezesha wakulima kuwa na masoko ya uhakika ya kuuza mazao ndani na nje ya nchi ili kujiongeza kipato na kuchangia zaidi katika pato la taifa.
 - i. Kuwezesha uanzishaji wa viwanda¹ vidogovidogo vya kusindika mazao vinavyotoa ajira kwa wingi kwa kuvifungamanisha na mnyororo wa uzalishaji vijijini .
 - j. Kuwezesha shule za Sekondari na vyuo vya ufundi kuwa kitovu cha kuonisha mafunzo na uzalishaji katika kuongezea mazao thamani.
 - k. Kutenga kiasi kikubwa cha fedha kwa ajili ya mikopo yenye masharti na riba nafuu, itakayoshindaniwa na vijana kwa ajili ya kupata mitaji na kuweza kujiajiri na kutoa ajira.
 - l. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi inakusudia kuweka msukumo katika uanzishwaji wa viwanda vikubwa katika kila Kanda ifikapo mwaka 2025 ili kuongeza thamani ya bidhaa tunazozalisha na kutengeneza ajira karibu na nguvu kazi ilipo .
 - m. Wanawake watawezesha ili kuanzisha vikundi vya kijamii vya kiuchumi na kuviendesha bila kupata bugudha na au kusumbuliwa na serikali katika kusajili, leseni za uendesaji

na kodi lukuki, hatua hii itawafanya wanawake ambao ndio wengi zaidi nchini kuwa ndio nguzo kuu ya uchumi katika familia na hatimaye jamii nzima.

- n. Ili kuongeza ufanisi na kupunguza msongamano katika Bandari ya Dar es Salaam, tutaimarisha bandari za Mtwara na Tanga kwa kuzifanya zifanye kazi kibiashara na kwa kuzingatia maslahi ya kitaifa. Aidha, tutaanza mkakati wa kuziunganisha bandari hizi tatu na nchi za jirani zitakazozihudumia; Bandari ya Mtwara kwa nchi za Kusini, Bandari ya Dar es Salaam kwa nchi za kati, na Bandari ya Tanga kwa nchi za Kaskazini.

4.1 SEKTA YA FEDHA

Sekta ya fedha iliyo imara katika nchi, ni nguzo imara katika kuhakikisha uchumi wa nchi unashamiri na unakuwa endelevu. Sekta binafsi iliyo imara inajengwa na sekta fedha, hivyo basi sekta hii ni muhimu sana katika kujenga uchumi.

Benki kuu ndio mlezi mkuu wa asasi na taasisi zote za fedha na pia ndio mamlaka ya mwisho ya kuhakikisha inatunga sera zote za fedha za ndani na za nje kwa mustakabali mwema wa uchumi wa nchi yetu.

Tanzania imekuwa na bahati njema sana kwa kuwa na mabanki mengi sana, lakini kuna changamoto kubwa kwa wananchi kupata mikopo kwa ajili ya kuanzisha na kuendeleza biashara hizo.

Changamoto kubwa kwa biashara mpya ni kupata fedha za kuanzia au mitaji, licha ya kuwa na mabanki mengi kumekuwa na vikwazo vingi na vikubwa kwa wajasiriamali wapya kwenye soko katika kupata mitaji. Jambo hili kwa upande mmoja ndio kisababishi kikubwa cha uwepo wa kundi kubwa la vijana wasiokuwa na ajira hapa nchini. Taasisi za fedha kuwa bega kwa

bega na sekta binafsi ndio linatakiwa kuwa kimbilio la Serikali katika kuhakikisha uchumi wa nchi unakuwa salama.

Changamoto hizo zinatokana na sera za fedha zinazotolewa na benki kuu kwa taasisi za fedha na hivyo kuwa ni kikwazo kikuu kwa mabanki kuweza kukopesha wajasiriamali wapya.

Chadema kwa kuona fursa zilizopo kwa taasisi za fedha hasa mabanki katika kujenga uchumi wa nchi inatarajia kufanya yafuatayo;

- a. Chadema itahakikisha kuwa inakuwa na sera za kifedha ambazo zitaiondoa nchi katika hatari kubwa ya madeni ya ndani na nje.
- b. Chadema itahakikisha inaimarisha mfumo mzima wa fedha na unakuwa shirikishi ili kuepuka uwezekano wa kushambuliwa na uhalifu wa kimtandao.
- c. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itatunga sera za kuwawezesha wananchi kushiriki na kunufaika na biashara ya masoko ya fedha inayotumia mitandao(*ushiriki wa masoko ya hisa ya kimataifa kwa kutumia mitandao*)
- d. Chadema itahakikisha kuwa kunakuwa na urahisi wa upatikanaji wa huduma za benki na fedha kwa ajili ya kusaidia wananchi kukuza biashara zao.
- e. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba Benki Kuu inatunga sera ambazo taasisi za fedha hasa benki kuwa na vitengo vya masoko na usimamizi kwa miradi yote ambayo wanaikopesha au inatekelezwa kwa kutumia fedha za mikopo.
- f. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba taasisi za fedha zinakuwa ni sehemu ya kutoa motisha kwa wananchi kutumia taasisi hizo katika kupambana na umasikini.

- g. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba kipaumbele cha kwanza kwa taasisi za fedha kiwe ni kuhudumia wananchi kabla ya kuhudumia Serikali.
- h. Serikali ya Chadema itaanzisha maeneo maalum (Kisiwa cha Mafia na Pemba) ya mitaji isiyotozwa kodi (tax heaven) ili kupanua wigo wa kupata mitaji kwa ajili ya miradi mikubwa na wajasiriamali wadogo.

4.2 MFUMO WA KODI RAFIKI KWA Wawekezaji Na Wafanyabiashara.

Imekuwa ni changamoto kubwa miongoni mwa wananchi, Makampuni na Wawekezaji wa ndani na nje katika kufanya biashara na hasa kutokana na kodi kubwa na tozo mbalimbali ambazo zimepelekea Biashara nyingi kufungwa, kushindwa kuanzishwa kwa biashara mpya, walipa kodi wa kati na wakubwa wakitangaza kupata hasara na hivyo kulazimika kupunguza baadhi wafanyakazi wake.

Aidha Manunuzi ya nje(imports) yamezidi kushuka, sekta ya nyumba(real estate) inazidi kuporomoka, kampuni zinazidi kupunguza wafanyakazi, soko la mitaji(stock market) linazidi kufanya vibaya, hali inayopelekea wawekezaji wengi kushindwa kuingiza mitaji yao na au kusimamisha baadhi ya miradi mipya ambayo ilikuwa tayari imeiva .

Hali hii inatokana na mfumo wetu wa sheria na sera za kodi na tozo mbalimbali ambao hazitabiriki na hubadilika badilika kila mara na hivyo kutishia mitaji ya wawekezaji kuwa hatarini kupotea.

Mfumo wa kodi uliopo sasa ni mfumo ambao unafilisi wafanyabiashara na wawekezaji kutokana na ulivyo mfumo kandamizi na umekuwa kishawishi kikubwa cha Rushwa kwa watoza kodi na walipa kodi.

Kwa mfumo wa sasa wa kodi ukianzisha biashara Tanzania unakumbana na utitiri wa masharti ya kodi na tozo mbalimbali kama ifuatavyo:-

- a. Utatakiwa kuisajili biashara yako au kampuni yako Brela.
- b. Utatakiwa kulipa kodi ya mapato (Income Tax) – TRA
- c. Utatakiwa kulipa kodi ya zuio (Withholding Tax)
- d. Utatakiwa kulipa kodi kadiri unavyopata kwako na kwa wafanyakazi wako – Pay As You Earn (PAYE)
- e. Utatakiwa kulipa gharama za OSHA – Occupational Service and Health Administration
- f. Utatakiwa kulipa kodi ya ujuzi (Skills Development Levy)
- g. Utatakiwa kulipia leseni ya Biashara katika Manispaa
- h. Utatakiwa kulipia gharama za zima moto (Fire)
- i. Utatakiwa kulipa ada za Mamlaka ya Chakula na Dawa (TMDA) – kwa ajili ya ukaguzi wa bidhaa moja (Product Inspection) ya dola za kimarekani 350.
- j. Kulipa gharama za GS1 kwa ajili ya alama ya kutambua bidhaa (Bar code)
- k. Kulipia vyeti vya TBS (kwa mfano bakery kwa mwaka wanalipa shilingi 2,500,000/=
- l. Utatakiwa kuwa na EFD mashine (hizi huuzwa kwa fedha nyingi)
- m. Utatakiwa kulipia wafanyakazi wako michango ya hifadhi ya jamii PSSSF au mifuko mingine ya hifadhi.
- n. Utatakiwa kulipia Mfuko wa Fidua kwa Wafanyakazi (Workers Compensation Fund).

Mbali ya kodi hizo zinazokatwa wakati biashara zinaanza hata kabla ya biashara husika kuweza kusimama na hivyo kuporomosha mtaji, kuna kodi zingine ambazo ni:

- a. Kodi ya mapato ya makampuni
- b. Kodi ya zuio
- c. Kodi ya pato linalotokana na uuzaji wa rasilimali
- d. Kodi ya mapato ya mkupuo mmoja
- e. Kodi ya mapato ya mtu binafsi-PAYE
- f. Kodi ya Uchakavu katika rasilimali
- g. Kodi ya ongezeko la thamani (VAT)
- h. Ushuru wa stempu
- i. Ushuru wa forodha

Katika tathmini ya saba ya hali ya uchumi wa Tanzania iliyotolewa tarehe (11/01/2018 na Shirika la Fedha Duniani (IMF), ni kwamba hali ya uchumi wa Tanzania imekuwa ikipanda na kushuka na kwamba matazamio ya mwenendo huo yanaonyesha mashaka.

Kwa kuwa Chadema tunaamini katika kuimarisha sekta binafsi kwani ndiyo injini ya kuendesha uchumi hivyo ni lazima tuutazame upya mfumo wa kodi(Tax regime) kwa maana ya kuangalia viwango vya kodi, uratibu wa kodi na mawanda mazima ya matokeo ya kodi kwa wananchi.

Kwa kuwa Chadema inaamini kuwa mfumo mzuri wa kodi utawafanya wafanyakazi, wafanyabiashara wadogo, wa kati na wakubwa kulipa kodi kwa hiari na hivyo kuongeza wigo wa ulipaji wa kodi.

Baadhi ya maeneo ambayo Serikali ya Chadema itayafanyia kazi katika kurekebisha mfumo wa kodi ni yafuatayo:-

4.2.1 Kupunguza Kiwango cha kodi ya makampuni “Corporate Tax”

Kiwango cha kodi hii kisizidi asilimia 20 na kisiwe chini ya asilimia 15 ya faida ya mfanyabiashara au mwekezaji. Ukipunguza kiwango hiki unayaongezea makampuni na wawekezaji binafsi pamoja na wafanya biashara nafasi ya kukuza mitaji yao na kupanua uwekezaji wao nchini na hivyo kuajiri watazania wengi zaidi.

4.2.2 Kupunguza Kodi ya ongezeko la thamani(VAT)

Kodi hii mlipaji wake ni mlaji wa mwisho. Kodi itapunguzwa mpaka asilimia isiyozidi 15 lakini isiyopungua asilimia 10. Uwepo wa kodi hii unawaumiza walaji wa mwisho wa bidhaa na hivyo kupunguza uwezo wa manunuzi wa wananchi.

Kwa hiyo kupunguzwa kwake kutakuwa na faida nyingi ikiwemo kuwafanya wananchi wawe na akiba ya kutosha zaidi kwa ajili ya uwekezaji na matumizi yao.

4.2.3 Kodi ya Ardhi

Tanzania ina ardhi kubwa sana hivyo ni vizuri viwango vya kodi ya ardhi viwe vidogo sana ili kufanya watu wote hata watu wa kipato cha chini waweze kupima na kumiliki hati za mashamba na viwanja. Kutokana na uwepo wa kodi hii sehemu kubwa ya ardhi ya Tanzania haijapimwa na hivyo kuendelea kuikoshesha mapato serikali.

Serikali ya Chadema itaweka utaratibu wa kuwa na viwango vizuri vya kodi ya ardhi kwa wananchi ili kuweza kupima ardhi na kuwa na hati ambazo wanaweza kuzitumia kuingia mikataba na asasi za fedha kwa ajili ya kupata mitaji ya kuwekeza kwenye miradi mbalimbali ya Kilimo, Mifugo, Uvuvi na Mazao ya Misitu.

- a. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itahakikisha ardhi yote ya jumla na ardhi ya vijiji inapangwa na kupimwa bure bila mwananchi kutozwa gharama yoyote ili kuondoa migogoro ya ardhi nchini na kumwezesha kila mwananchi kulinda ardhi yake kikamilifu.
- b. Serikali ya Chadema itafuta tozo ya malipo ya mbele (Premium) inayotozwa kabla ya kupata hati ili kumwezesha kila mwananchi kupata hatimiliki ya ardhi yake kwa gharama nafuu, kulinda ardhi yake kisheria na kuweza kukopesheka kwa urahisi kwa dhamana ya hatimiliki yake, kodi hii inabeba zaidi ya 84% ya gharama zote za kupata hatimiliki ya ardhi.

4.2.4 Tozo zinazotozwa na taasisi, mashirika ya Serikali na Halmashauri nchini.

Mfumo wa kodi wa serikali itakayosimamiwa na Chadema utafanya uoanishaji (harmonization) mkubwa kwenye tozo za taasisi zake ikiwemo OSHA, NEMC, LATRA EWURA, FIRE, TMDA na TBS. Hizi Taasisi zinapaswa kuwa taasisi za kutoa huduma (services providers) na sio taasisi za kibiashara.

Serikali itakayoongozwa na Chadema itatoa ruzuku kwa ajili ya taasisi hizo kujiendesha na ili zisiwe vyombo vya kusitisha mori ya uanzishwaji na uwekezaji katika biashara na viwanda hapa nchini

4.3 UCHUMI WA KIDIGITALI

Uchumi wa kidigitali ni mfumo mpya wa kibiashara unaohusisha matumizi mapana ya teknolojia ya simu na kompyuta katika uuzaji na ununuzi wa bidhaa, ubunifu na ugunduzi unaofanywa na watu kwa kutumia maarifa na ujuzi katika matumizi madhubuti ya kompyuta na Wavuti ambayo inafanikisha miamala ya kifedha kununua na kuuza bidhaa kote duniani.

Kwa mujibu wa taarifa ya benki ya dunia ya mwaka 2016 inaonesha kuwa TEHAMA ilichangia takribani asilimia 17% ya pato la taifa kwa mataifa yanayoendelea. Aidha kwa mujibu wa taarifa ya UNCTAD-2015 kumekuwa na maendeleo makubwa kwa e-commerce kwa mataifa ya Asia ya Kusini na pia kwa mujibu wa world economic forum –WEF, 2015) uchumi wa mtandao (internet economy) ulikua kwa kiwango cha kati ya asilimia 15-25% kwa mwaka.

Kutokana na kasi kubwa ya ukuaji na mabadiliko makubwa ya kiteknolojia yanayoendelea ulimwenguni kwa sasa, ni lazima Tanzania ianze kujipanga ili iweze kunufaika na ukuaji huo kwa kuweka mikakati thabiti na endelevu ya kuwa na uchumi wa Kidijitali.

Kwa mantiki hiyo, serikali ya Chadema imepanga kufanya ifuatavyo;

- a. Kwa kushirikiana na sekta binafsi, serikali ya Chadema itaratibu upatikanaji wa miundo mbinu ya kisasa ya mitandao ya Kompyuta/simu (4G-5G) ili kufanikisha azima ya kushiriki katika uwanda wa uchumi wa kidigitali.
- b. Kwa kushirikiana na sekta binafsi, serikali ya Chadema itawezesha upatikanaji wa taarifa za mitaji, masoko, na uwekezaji kupitia jukwaa la biashara mtandaoni(e-commerce forum) ili kuwawezesha Wakulima, Wafugaji, Wavuvi na Wafanya biashara Wadogo kwa Wakubwa kuuza na kununua bidhaa zao ndani na nje ya nchi kwa kuanzisha mifumo ya kidigitali (Application- app) za umma na za binafsi
- c. Kwa kushirikiana na sekta binafsi, serikali ya Chadema itaanzisha mfumo wa malipo kwa kila hudumu inayotolewa na sekta zitoazo huduma hapa nchini

- kupitia mfumo wa malipo mtandaoni (online payment) utakao kuwa ukitumia kadi janja maalumu (smart card) au Application-app maalum (kwa mfano usafiri wa anga, majini, na nchi kavu, huduma za maji, umeme, pango la aridhi, hati mbali mbali, ada za masomo, faini za barabarani, faini za mahakamani)
- d. Kwa kushirikiana na sekta binafsi, serikali ya Chadema italinda haki zote za Wabunifu na Wazalishaji mali kupitia mtandao wa simu au kompyuta ili kukuza uzalendo na kuliongezea pato Taifa
- e. Kwa kushirikiana na sekta binafsi, serikali ya Chadema itaanzisha mafunzo rasmi ili kuwajengea Watanzania uwezo wa kufanya biashara kupitia mitandao ya simu na kompyuta. Mafunzo haya yatalenga utoaji huduma, uuzaji wa bidhaa na ununuzi wa bidhaa kupitia mifumo ya wavuti za internet na simu janja. Kwa kushirikiana na sekta binafsi, serikali ya Chadema itapeleka muswada rasmi wa uchumi wa kidigitali ili kutunga sheria, kanuni na taratibu za kuratibu uchumi wa kidigitali

5. ELIMU BORA KWA MAENDELEO ENDELEVU



Elimu bora ni ufunguo wa maendeleo endelevu, amani na utulivu. Elimu pekee ndio rasilimali ya kibinadamu ya Taifa inayoamua juu ya sura na kasi ya maendeleo ya kijamii na kiuchumi.

Umaskini mkubwa uliokithiri nchini unachangiwa kwa kiasi kikubwa na kiwango duni cha elimu. Chadema inaamini na inatambua kuwa elimu ni haki ya msingi ya binadamu. Tumefanikiwa sana kuwaandikisha watoto wetu shule kwa mamilioni (quantity) lakini bado hatujafanikiwa kabisa katika suala la ubora wa elimu (quality).

Serikali itakayoongozwa na Chadema katika mipango yake imekusudia kuinua kiwango cha elimu kwa kuipa kipaumbele namba moja, mbili na tatu. Ni matumaini yetu kuwa Tanzania itakuwa kitovu cha elimu bora katika Afrika ya Mashariki na Kati.

5.1 MSONGAMANO WA WANAFUNZI

Mfumo wetu wa elimu unaanzia shule ya awali hadi vyuo vikuu. Kwa bahati mbaya sana shule zetu hasa za awali na msingi zina uhaba mkubwa wa miundombinu ya madarasa, vyoo, maabara na maktaba. Hali hii imepelekea kuwa na msongamano mkubwa sana katika madarasa. Leo tuna wastani wa wanafunzi 100 kwa darasa moja badala ya 45 kama inavyoelekezwa.

Hali hii haiwezi kumfanya mwanafunzi awe msikivu darasani wala mwalimu kufundisha kwa weledi na utulivu. Wengi wa wanafunzi wanakaa kwenye sakafu (udongo) na wengine kwenye mawe kwa ukosefu wa madawati, na mbaya zaidi sakafu zenyewe zina vumbi kiasi cha kuathiri afya za wanafunzi na uchafu kwa sare za wanafunzi. Kwenye maeneo mengine wanafunzi wa madarasa mawili tofauti wanasomea darasa moja kwa wakati mmoja. Hali hii inapelekea wanafunzi kuhitimu elimu ya msingi bila kujua kusoma na kuandika.

5.2 MASLAHI YA WALIMU

Elimu ni mwalimu, kwani unaweza kuwa na madarasa mazuri sana, maabara ya viwango vya juu lakini bila mwalimu mwenye motisha na aliyepewa mafunzo vizuri hakuna chochote tutakachofanikiwa. Elimu ni sawa na kiwanda ambapo mwanafunzi ni malighafi; walimu na vitabu ndio mashine za uchakataji na usindikaji. Hivyo kama ilivyo kwa malighafi inapopita kwenye mashine tunachopata ni kitu kipya kama pamba kuwa nguo, zabibu kuwa mvinyo n.k. Hivyo mtoto anaingia hajui chochote lakini anategemewa atoke amebadilika kwa kujua kusoma, kuandika na kubwa zaidi kujitambua na kujua kuchambua mambo.

Elimu ya ualimu inayotolewa haina ubora wa kutosha kwa kuwa elimu hiyo ndio inayotegemewa katika kuwafundisha watoto wetu. Walimu hawathaminiwi kabisa; mishahara, maslahi na marupurupu yao hayalingani na kazi ngumu wanayoifanya ya

kulielimisha Taifa na kulijengea msingi wa maendeleo. Mbaya zaidi, kuna upungufu mkubwa wa walimu wa masomo hususan masomo ya kiingereza, hisabati na sayansi ambayo ni muhimu mno kwa ulimwengu huu wa sayansi na teknolojia.

5.3 VIFAA VYA KUFUNDISHIA NA KUJIFUNZIA

Hali ya vifaa katika shule zetu nyingi za sekondari inasikitisha sana. Maabara ambazo ndio sehemu ya kufanya majaribio ya sayansi ni chache mno na kama zipo basi hazina vifaa vya kutosha ama kukosa walimu wenye sifa. Kuna upungufu wa kutisha wa vitabu vya kufundishia katika shule zetu. Pamoja na dunia kubadilika na kuongezeka kwa mahitaji ya elimu ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA), bado shule zetu hazina kompyuta wala hazijaunganishwa na mkongo wa Taifa kwa ajili ya intaneti.

5.4 MFUMO WA ELIMU NA MITAALA

Ni ukweli ulio wazi kuwa mfumo wetu wa Elimu umepitwa na wakati. Mfumo wetu wa elimu kwa muda mrefu umeonesha udhaifu katika usimamizi, uendeshaji, uhibitaji na ugharimiaji tangu Taifa letu lilipoamua kufanya ugatuzi wa madaraka, uliophelekeasektaya elimu kuendeshwa chini ya wizara tatu tofauti. Wizara inayoshughulikia elimu imeachiwa sera pekee, wakati ajira za waalimu zinasimamiwa na wizara inayoshughulikia utumishi na wizara ya tawala za mikoa na Serikali za mitaa. Mfumo huu umetuletea matokeo yasiyoridhisha. Ni wazi kuwa watoto wetu wanaanza shule ya msingi kwa kuchelewa sana na wanakaa shuleni kwa muda mfupi.

Kiwango cha wastani duniani cha muda wa kusoma shuleni ni miaka 9 lakini wa kwetu ni miaka 7 pekee. Matokeo yake watoto wetu wanamaliza shule wakiwa wadogo na bila kuwa na maarifa na stadi za msingi za kuwafanya wajitegemee. Mitaala ni mikubwa mno na haizingatii mahitaji ya mwanafunzi na mazingira yetu. Bado imejikita kwenye mfumo wa kikoloni na

haiendani na mahitaji yetu ya sasa na malengo ya kiuchumi na kimaendeleo ya jamii tunayokusudia kujenga. Mabadiliko ya mitaala hayaendi sambamba na matayarisho ya walimu na maendeleo ya vitabu vya kusomeshea. Hakujatolewa mkazo unaostahili wa elimu ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).

5.5 ELIMU YA JUU

Elimu ya juu ndio inayomfunza kijana jinsi ya kuchambua mambo na kujenga weledi katika fani mbalimbali. Mwl. Nyerere, katika kitabu chake cha Uhuru na Maendeleo, alisema: *“Wasomi wana mchango maalum wa kutoa katika maendeleo ya Taifa letu, na kwa ujuzi wao na uelewa mkubwa wanaopaswa kuwa nao utumike kwa manufaa ya jamii ambayo wote ni wajumbe”*. Tumeshuhudia maneno haya mazuri ya Hayati Baba wa Taifa yakipuuzwa kwani mchango wa wasomi wetu katika maendeleo ya jamii na taifa kwa jumla umewekewa vikwazo na mfumo wa utawala wa Serikali hii ya CCM. Elimu ya juu kwa Taifa lolote ni muhimu kwa sababu inalenga katika kuwaandaa wataalamu wa fani tofauti kuja kukabidhiwa majukumu mbali mbali kwenye jamii.

5.5.1 Hali ya Vyuu Vikuu

Vyuu Vikuu vyetu vinakabiliwa na hali ngumu ya upatikanaji wa Wasomi wakiwemo wahadhiri katika taasisi zetu za elimu ya juu wamekuwa wakiondoka kwenda ughaibuni na wengi kuteuliwa kushika nyadhifa za kisiasa na za kiserikali kutokana na maslahi duni wanayopata hapa nchini. Katika vyuu vyetu vyote vya elimu ya juu, huduma za kitafiti bado zinalegalega na hazijapewa umuhimu kutokana na kushindwa kutenga fedha kwa shughuli hiyo.

5.5.2 Bodi ya Mikopo

Kuundwa kwa Bodi ya Mikopo ya elimu ya juu hakujasaidia kuondoa tatizo la wanafunzi kushindwa kuendelea na

masomo yao. Kundi kubwa la wahitimu wa kidato cha sita wenye sifa limekua likikosa mikopo ya kuendelea na masomo. Hata hivyo bado vigezo vya utoaji wa mikopo kwa wanafunzi hauzingatii hali halisi ya maisha na uwezo wa kifedha wa wazazi wa wanafunzi.

Ugharamiaji wa elimu ya juu ndio changamoto kubwa kwenye elimu ya juu na hivyo kusababisha watu wenye sifa za kusoma kushindwa kupata ufadhili wa Serikali. Kwa muktadha huo Serikali ya Chadema inasema kuwa itahakikisha wale wote wenye sifa za kujiunga na vyuo vya kati, vyuo vya ufundi na vyuo vikuu wanapewa mikopo bila ya ubaguzi wowote.

Kwa kuwa fedha hizo ni za mikopo na sio bure, hivyo basi Serikali italazimika kupunguza kiwango cha marejesho ya mikopo ya elimu ya juu hadi kufikia asilimia tatu (3) ya mshahara wa mnufaika na kutanua wigo wa muda wa marejesho hadi kufikia miaka 25 tangu mnufaika apate ajira.

Aidha, Serikali itafuta riba na tozo zote zitokanazo na adhabu ya kuchelewesha marejesho ya mikopo wa elimu ya juu. Lengo kuu la kupunguza kiwango cha marejesho na kuongeza muda wa kulipa ni kuweka mazingira wezeshi ili kila mhusika alipe na usiwe mzigo wa kumfanya asiweze kuwekeza katika shughuli zingine za uzalishaji.

5.6 UWEKEZAJI KATIKA LUGHA YA KUJIFUNZA NA KUFUNDISHIA

Umuhimu wa mwanafunzi kuelewa kwa ufasaha lugha anayotumia kujifunzia na ule wa mwalimu kuwa na weledi katika lugha anayotumia kufundishia haupewi uzito unaostahili. Ni kawaida kukuta mwalimu darasani akifundisha kwa lugha ambayo hata yeye mwenyewe haijui vizuri na wanafunzi kutahiniwa katika hali hiyo hiyo.

Lugha ya kiingereza mathalani, ndiyo lugha ambayo inatumika kufundishia na kujifunza kwa masomo yote (Ukitoa somo la Kiswahili) kwa ngazi ya sekondari hapa nchini. Lakini cha ajabu ni kwamba imekuwa ni kawaida kukuta walimu na wanafunzi wakiwa na ujuzi mdogo wa lugha hii ambayo tumeruhusu itumike. Hali hii inapelekea wanafunzi kushindwa kabisa kuizungumza kwa ufasaha hata kwa wale wenye PhD.

5.7 MPANGO WA MAENDELEO WA MIAKA 5 KATIKA ELIMU UMEFIFISHA SEKTA YA ELIMU.

Wakati mataifa mengine yapo mbele yetu katika Sekta ya elimu, yanakimbia kwa kasi isiyo ya kawaida katika ubunifu na teknolojia, hapa nchini Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa miaka 5, inapendekeza nchi hii itembeke taratibu katika mapitio ya elimu ya msingi na elimu ya sekondari. Suala hili Halikubaliki.

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa miaka 5, unapendekeza ugharimaji wa Maendeleo ya elimu ya msingi uwe Shilingi Bilioni 1,357 ambazo ni sawa na asilimia 28% ya fedha zote zinazotarajiwa kutengwa kwa miaka yote mitano (Bilioni 4,898.92.) wakati huo huo mikopo ya elimu ya juu pekee ikitengewa jumla ya Shilingi Bilioni 2,500 ambazo ni sawa na asilimia 51% ya fedha zote zinatakazotengwa katika sekta ya elimu. Mfumo huu unatenga fedha nyingi za Maendeleo katika elimu ya juu pekee huku idara nyingine zikipata fedha kidogo sana na haya ndiyo matokeo ya changamoto nyingi kwenye elimu ya awali hadi sekondari.

Serikali itakayoongozwa na Chadema itafanya yafuatayo:

- a. Itajenga shule mpya za kisasa na kuongeza madarasa kadiri inavyohitajika ili kuondoa msongamano
- b. Itatenga fedha kila mwaka kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ili ndani ya miaka mitano tatizo liwe limepungua au kuisha kabisa.

- c. Itaanzisha utaratibu wa kufanya tathmini na ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha ubora wa elimu inayotolewa.
- d. Itafanya jitihada maalum kwa kutoa chakula shuleni ili kuwavutia wanafunzi kuendelea na masomo na hivyo kupunguza idadi ya wanao katiza masomo.
- e. Itapanua wigo wa elimu ya msingi ili watoto wakae shuleni kwa muda usiopungua miaka tisa kama ilivyo katika viwango vya kimataifa
- f. Itaunganisha Elimu ya msingi na elimu ya mafunzo ya ufundi ili kwamba vijana wetu wamalizapo elimu ya msingi wawe na maarifa na stadi za kufanya kazi itakayowafanya wajitegemee popote walipo.
- g. Itaboresha na kujenga miundombinu ya elimu ili watoto wafurahie masomo yao
- h. Itaboresha Maslahi ya walimu ikiwa ni pamoja na kuwapandisha madaraja kwa wakati
- i. Itaanzisha Wakala wa ukaguzi wa shule ili kuhakikisha Ukaguzi wa Shule za Msingi na Sekondari nchini zinakaguliwa kwa kiwango cha kuridhisha.
- j. Itahakikisha fedha za ruzuku kwa wanafunzi zinafika kwa wakati.
- k. Itawekeza katika kuwajengea weledi wa lugha walimu, kwa kutenga bajeti maalumu na kuwapa mafunzo maalumu ya lugha ya kiingereza
- l. Itaweka wazi ajira ya walimu kufuatana na mahitaji ya elimu na kupitia mitihani ili kuhakikisha wanaajiriwa walimu wenye sifa zinazohitajika.
- m. Itatekeleza kikamilifu Kanuni za Utumishi wa Walimu na kwa uwazi kabisa itazienzi na kuheshimu juhudi za walimu.

- n. Itafanya mazungumzo na nchi washirika wa maendeleo na mashirika ya kimataifa kama vile PeaceCorps kwa ajili ya kuendelea kupatiwa walimu wa kutosha wa masomo ya kiingereza, hisabati na sayansi.
- o. Itaanzisha na kusimamia kikamilifu mpango kwa shule zote za sekondari kuwa na Maktaba za kisasa za kuwahudumia wanafunzi na kukuza vipaji vyao vya kujisomea na kujiendeleza.
- p. Itaiimarisha Maktaba Kuu ya Serikali kwa kuiongezea hadhi na uwezo na kuipatia vitabu na machapisho yote muhimu na pia itaanzisha na kuziimarisha Maktaba za Mikoa na Wilaya ili kusogeza huduma hizi kwa wananchi wote wakiwemo wale wa vijijini.
- q. Itahakikisha kuwa shule zote za sekondari zinapatiwa maabara zenye vifaa na walimu (lab Technicians).
- r. Itazipatia kila shule za sekondari kompyuta za kutosha kwa ajili ya kukuza elimu ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA).
- s. Itafanya mapitio ya mitaala ili iendane na mazingira na uhalisia wa soko la ajira
- t. Itahakikisha kuwa elimu na mafunzo ya teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) vinapewa nafasi kubwa katika mitaala ya masomo kuanzia ngazi ya shule za awali hadi vyuo vikuu.
- u. Itaweka utaratibu utakaowawezesha vijana wote wenye sifa na waliochaguliwa kujiunga katika chuo kikuu chochote ndani ya nchi wanapata elimu ya juu bila vikwazo.
- v. Itagharamia mahitaji yote (bursaries) kwa wanafunzi angalau 50 waliofanya vizuri zaidi mitihani yao ya mwisho ya kidato cha Sita kusoma kwenye vyuo mashuhuri duniani ili watoe motisha kwa wenzao

kufanya vizuri lakini pia kuleta uzoefu wa nchi hizo.

- w. Itatengeneza mtandao mzuri wa matumizi ya intaneti katika vyuo vikuu vyote vya Serikali na kuhakikisha kuwa panakuwa na kompyuta za kutosha
- x. Itahamasisha na kuziunga mkono juhudi za watu binafsi, mashirika ya dini, na taasisi nyingine zenye malengo ya kuanzisha vyuo vikuu kwa ajili ya taaluma mbali mbali, lengo likiwa ni kuifanya Tanzania kuwa kituo kikuu cha elimu na mafunzo katika eneo la Afrika Mashariki na Kati.
- y. Itaanzisha kitengo maalumu cha kuratibu na kuzifanyia kazi tafiti/vumbuzi mbalimbali zinazopatikana kutokana na jitihada zilizofanywa katika vyuo vyetu kwa lengo la kusaidia ukuzaji wa uchumi na maendeleo na ustawi wa nchi yetu na watu wake.
- z. Itaanzisha mazungumzo na taasisi za dini na taasisi mbalimbali zilizokuwa zinamiliki shule lakini zikataifishwa na Serikali, hivyo kuzirejeshea umiliki na uendeshaji wa shule zao.

6. AFYA, HIFADHI NA HUDUMA ZA JAMII



Chadema inakubaliana na tafsiri ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kwamba *“Afya ni hali yakutokuwa na maradhi na ukamilifu wa binadamu kiakili, kimwili na kijamii”*

CHADEMA inatambua pia kwamba afya bora ni nguzo muhimu kwa ajili ya maendeleo ya mtu binafsi, familia na taifa. Kwa sababu hiyo, Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itawekeza katika sekta ya afya ili kulinda nguvu kazi ya taifa na hivyo kuwa na maendeleo endelevu.

Ni ukweli kwamba huduma bora ya afya hapa nchini imekuwa ni bidhaa adhimu kuweza kupatikana kutokana na mazingira ambayo sio rafiki (changamoto nyingi) kuanzia kwenye miundombinu, rasilimali watu hadi huduma yenyewe. Mpaka sasa hakuna uwiano sawia wa vituo vya kutolea huduma za afya na idadi ya watumia au wahitaji wa huduma, alikadharika watendaji/ wahudumu na wahudumiwa.

Hivyo basi, Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itafanya yafuatayo katika kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma bora ya afya;

- a. Itajenga, itaendeleza na kutumia miundombinu ya afya kwa kutumia mfumo wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP)
- b. Itaongeza udahili wa mafunzo ya watendaji katika sekta ya afya ili kukidhi mahitaji ya jamii kupitia ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma lakini Serikali ikibaki kuwa mbia mkuu.
- c. Itatoa motisha kwa watendaji wa Sekta ya afya kulingana na nafasi zao kiutendaji.
- d. Itatoa upendeleo wa makusudi wa kukuza matumizi ya teknolojia za kisasa katika kutoa huduma kwenye afya.
- e. Itaimarisha Baraza la Taifa la Utafiti wa Kitabibu kwa kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya tafiti za kitabibu na kuzitoa kwa wakati.
- f. Itahakikisha kwamba inasajili taasisi za ndani za utafiti wa kitabibu, tiba asili na tiba mbadala kwa ajili ya kuboresha sekta ya afya nchini.
- g. Itaboresha mifumo ya huduma za dharura katika maeneo yote ya utoaji wa huduma za afya ili kupunguza idadi ya vifo vinavyotokea kabla ya kufika katika vituo vya afya.
- h. Itahimiza sekta binafsi kuwekeza katika kuanzisha huduma ya usafiri kwa wagonjwa katika hospitali za umma.
- i. Itaanzisha mchakato wa kujitathimini kwa wahudumu wa afya kwa ajili ya maisha yao hapa Tanzania, viwango vyao vya maslahi, na ubora kwa ajili ya utoaji wa huduma,
- j. Itatilia mkazo umuhimu wa dawa na huduma nyingine za kitabibu katika kutoa huduma bora za afya kupitia ubia kati ya sekta binafsi na sekta ya umma;

- k. Serikali itawezesha sekta binafsi kuwekeza katika uzalishaji wa dawa na huduma nyingine za kitabibu hapa nchini.
- l. Itahakikisha kwamba, mfumo wa usambazaji wa vifaa tiba, dawa, vitendanishi na bidhaa nyingine za kitabibu hauingiliwi kupitia njia ya ugatuaji.
- m. Serikali ya Chadema itatoa ruzuku kupitia mpango wa ustawi wa jamii kwa huduma za matibabu ya kibingwa na upasuaji kwani yana gharama kubwa na watu wengi hawawezi kumudu gharama hizo.
- n. Itathamini vipaji na itatoa uwanja mpana kwa Madaktari, Wauguzi na Wahudumu wengine katika sekta ya afya wakiwemo wanaohudumu katika sekta ya umma kuendesha shughuli zao binafsi za utoaji wa huduma ya afya huku Serikali ikiwasaidia kutoa huduma bora zenye viwango vya hali ya juu katika hospitali za umma.
 - Itanzisha mfumo imara wa ustawi wa jamii ambao utasaidia kuwapatia wananchi wote bima ya afya bila ya ubaguzi wa aina yoyote.

6.1 HIFADHI NA HUDUMA ZA JAMII

Hifadhi ya Jamii ni moja ya haki za binadamu inayotambuliwa kimataifa na Tanzania imekwisharidhia. Shirika la kazi duniani linatafsiri hifadhi ya jamii kama njia zote ambazo jamii hutumia kulinda watu wake na adha zote zitokanazo na hali ngumu ya kiuchumi na kijamii.

- a) Kila Mtanzania, lazima apate Chakula, Makazi na Huduma bora za jamii
- b) Kinga za kijamii, kusimamia mpango wa pensheni na mafao ya uzeeni kwa wazee wote.
- c) Bima na kinga mbali mbali ikiwemo bima ya afya

Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa;

- a. Mifuko ya hifadhi iliyoanzishwa baada ya kutungwa kwa sheria mpya ya kusimamia tasnia ya hifadhi ya jamii zinatumiwa kikokotoo (formula) kilichokuwa kinatumiwa kulipa mafao ya wastaafu na mifuko husika kabla ya kuunganishwa kwa mifuko husika.
- b. Itahakikisha inapanua wigo wa wachangiaji kwenye mifuko ya jamii.
- c. Wazee wote kulipwa pensheni na kuwa na uhakika wakupata matibabu bila malipo kwa wazee wote.

6.2 HUDUMA KWA WATU WENYE MAHITAJI MAALUM

Lengo kuu la Serikali ya Chadema kuhusu watu wenye mahitaji maalumu ni kuwawezesha kuishi maisha bora ili waweze kutoa mchango wao katika jamii kama walivyo Watanzania wengine. Serikali ya Chadema itachukua hatua zifuatazo katika kuboresha hali za maisha kwa watu wenye ulemavu.

- a. Kuhakikisha kuwa sheria ya kutobagua watu inatiliwa mkazo kwa kuongeza mabadiliko kuhakikisha kuwa Watanzania wote ambao wana mahitaji maalumu (kama vile ulemavu) na bado wana uwezo wa kushiriki katika shughuli mbalimbali za ujenzi wa Taifa wanapewa nafasi hiyo bila ubaguzi wa aina yoyote ile kwa kadiri ya uwezo wao.
- b. Kuharakisha uanzishwaji wa mfuko maalumu kwa ajili ya watu wenye mahitaji maalumu ambao utawawezesha kushiriki katika fursa za kiuchumi kwa njia ya mikopo.
- c. Kutoa mafunzo maalumu kuhusu stadi za maisha kwa watu wenye mahitaji maalumu kupitia vyuo vya ufundi stadi, vya serikali na binafsi kupitia mpango wa PPP. Mafunzo haya yatagharamiwa moja kwa moja na serikali kupitia wizara husika

- d. Kuhakikisha kuwa kuna vifaa muhimu kwa mahitaji ya watu wenye mahitaji maalumu mashuleni na sehemu zingine za mafunzo. Hii ni pamoja na kuhakikisha kuwa mashule, vyuo na sehemu zote za huduma kwa umma zinazingatia ujenzi wa majengo yanaweza kufikika na watu wenye mahitaji maalumu, kama vile ulemavu.
- e. Kuhakikisha kuwa miundombinu yote muhimu ikiwemo Majengo na barabara inatengenezwa na kurekebisha ili kukidhi na kuzingatia mahitaji ya watu wenye mahitaji maalumu.
- f. Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa watu wote wenye mahitaji maalumu ambao kutokana nao hawawezi kabisa kujipatia kipato wanaishi kwa gharama ya umma. Katika kutimiza hili, tutahakikisha kuwa familia zenye watu wenye mahitaji maalumu wa aina zote zinapatiwa huduma mbalimbali za afya bure na kwa kushirikiana na vyama mbalimbali vya kijamii, pia serikali itapitia na kuandika upya sera ya watu wenye mahitaji maalumu ili kuhakikisha kuwa hakuna Mtanzania yeyote mwenye mahitaji maalumu anayekosa huduma muhimu za jamii, kama afya, elimu, ajira, chakula au makazi.

6.3 MPANGO WA CHADEMA KUHUSU WANAWAKE NA WATOTO

Serikali ya Chadema itafanya yafuatayo ili kuhakikisha kuwa ustawi wa Wanawake na watoto nchini:

- a. Itahakikisha kuwa unyanyasaji wa wanawake katika masuala ya mirathi na talaka unakomeshwa kwa kushirikiana na wadau mbalimbali kama vile taasisi za dini na mashirika ya kijamii.
- b. Haki za watoto zitazingatiwa ikiwepo haki ya kuishi katika mazingira ya amani, kusoma na kupatiwa mahitaji muhimu anayostahili.

- c. Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa inawalinda watoto dhidi ya kutumikishwa na hasa kwenye machimbo ya madini, viwandani na kwenye mashamba makubwa , itakuwa ni kosa la jinai kumtumikisha mtoto nchini.
- d. Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa mtoto wa kike aliyepata ujauzito akiwa masomoni anakuwa na haki ya kurejea masomoni mara atakapojifungua .
- e. Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa wanawake wanapata fursa sawa za ajira na kulipwa ujira sawa na mwanaume kama wanafanya kazi zinazofanana .
- f. Serikali ya Chadema itaandaa na hatimaye kupitisha Sheria yenye kuzuia na kukabiliana na matumizi ya nguvu majumbani na ya vuguru za kijinsia (*Gender Based Violence Act*). Licha ya kutungwa kwa sheria hiyo, Serikali ya Chadema itachukua hatua zingine ili kukabiliana na tatizo hili ambalo ni kubwa katika jamii yetu. Hatua hizi ni pamoja na:
 - a. Kufanyia mabadiliko sheria ya Ndoa ili kuhakikisha kuwa ubakaji ndani ya ndoa unatambulika kuwa ni kosa la jinai.
 - b. Kulinda watumishi wa ndani na wasaidizi wa majumbani dhidi ya matumizi ya nguvu na unyanyasaji wa kijinsia.

6.4 FURSA ZA AJIRA NA UJIRA BORA KWA VIJANA

Kwa mujibu wa takwimu zilizotolewa na Umoja wa Mataifa za mwaka 2017 zinaonyesha kuwa vijana ulimwenguni ni takribani Bilioni 1.8, na kati yao vijana zaidi ya 600 Milioni wanaishi kwenye maeneo tete yenye machafuko na wengine zaidi ya 400 Milioni hawapati huduma muhimu za afya.

Kwa mujibu wa taarifa ya Ofisi ya Waziri Mkuu alipokuwa akiwasilisha bajeti ya mwaka 2015/16 ilieleza kuwa idadi ya vijana nchini ni 16.2 Milioni ambao ni sawa na asilimia 35.1

ya watu wote nchini. Kati ya jumla hiyo, asilimia 30 wanaishi vijijini kwa kutegemea kilimo ambacho kwa ujumla wake kimeajiri asilimia 60.3 ya vijana wote nchini.

Serikali ya CCM, imeshindwa kutengeneza mazingira bora kwa vijana wengi ili wape ajira inayoweza kutoa ujira stahili, kwani;

- a) Vijana wengi hawana elimu inayoendana na soko la ajira, iwe kwa kuajiriwa au kujiajiri.
- b) Vijana wengi wanaojihusisha na kilimo wanashindwa kukifanya kilimo kuwa cha kisasa cha kibiashara na endelevu.
- c) Kwa kipindi cha miaka 5 iliyopita serikali imeshindwa kuajiri vijana wake ambao wamemaliza masomo katika fani mbalimbali pamoja na upungufu wa watumishi uliopo Serikalini.
- d) Takriban asilimia 21 ya vijana wote nchini ndio wanaojiunga na elimu ya sekondari, hii ni idadi ndogo sana na matokeo yake imeacha takriban asilimia 79 ya vijana mitaani bila kuingia katika mfumo rasmi wa elimu ya sekondani au wa elimu ya ufundi na stadi za kazi.

Serikali ya CHADEMA itahakikisha kuwa:

- a. Itatoa na kuimarisha elimu ya ufundi na stadi za kazi mashuleni, ili hatimaye mwanafunzi atakapohitimu masomo yake anakuwa na uwezo wa kujiajiri kwenye fani ya ufundi na uongezaji wa thamani kwa mazao ya kilimo badala ya kusubiria ajira rasmi kutoka serikalini.
- b. Itahakikisha kunakuwepo na mashamba yenye miundombinu ya umwagiliaji kwa ajili ya kilimo cha mboga mboga ili vijana waweze kujihusisha na kilimo.
- c. Kujenga viwanda vya kuchakata mazao katika kila Mkoa na hata wilaya, viwanda hivi vitasaidia kuongeza fursa

- za ajira na kuongezea thamani mazao ya wakulima.
- d. Kupitia upya mfumo wa ujira ili kuhakikisha kuwa waajiriwa wanapata ujira unaokidhi mahitaji ya maisha kama vile nyumba, chakula na mavazi.
 - e. Kima cha chini cha mshahara lazima kimwezeshe mfanyakazi kuweka akiba isiyopungua asilimia 5 ya ujira wake, hili litaenda sambamba na Kuweka uwiano mzuri wa mishahara kati ya kima cha chini na juu na kupunguza kusigana baina ya mishahara.
 - f. Kupunguza tozo kwenye mshahara (PAYE) na kuwa si zaidi ya asilimia 8. Aidha serikali itahakikisha kuwa makato anayokatwa mfanyakazi kama vile kulipia madeni ya Bodi ya Mikopo, Bima ya Afya, mifuko ya hifadhi ya jamii na mengineyo hayatazidi asilimia 30% ya mapato ghafi ya mfanyakazi.
 - g. Chadema itaweka utaratibu kwa kila Halimashauri nchini kuwa na kanzi data ya vijana kuweza kujiandikisha juu ya taaluma zao na hivyo kuwa na senta moja ya utambuzi wa vijana ambao hawana ajira na pindi fursa itakapopatikana kulingana na uwezo na au taaluma ya kijana husika wataweza kujulikana na kuajiriwa, na hii itaondoa upendeleo na kujuana katika kutoa ajira kwani wataajiriwa kulingana na sifa na yupi alitangulia kujiandikisha.
 - h. Chadema itaweka utaratibu wa kisheria kwa ajili ya taasisi zote za fedha zitakazokuwa zinatoa mikopo kwa masharti nafuu kwa vijana kupatiwa motisha na serikali kama vile kupunguziwa baadhi ya kodi au ushuru kwa lengo la kuziwezesha kuwa na mitaji mikubwa ili vijana wengi zaidi waweze kunufaika na mikopo husika .

7. ARDHI, MAJI, MIPANGO MIJI, NYUMBA NA MAENDELEO VIJIJINI

Taifa letu kwa miongo kadhaa linaendelea kukumbwa na migogoro ya ardhi inayoendelea kuibuka mara kwa mara baina ya wananchi, mamlaka kwa mamlaka (mfano Kijiji kimoja na Kijiji kingine, au Kijiji na Mamlaka ya Hifadhi), Wananchi na mamlaka za hifadhi, migogoro ya wafugaji na wakulima pamoja na migogoro kati ya wananchi na wawekezaji.

Pamoja na changamoto hizo bado kwa miaka mitano iliyopita Serikali haijachukua hatua madhubuti kupima ardhi nchini ikiwa ni pamoja na kutenga maeneo kwa ajili ya makundi yaliyoko kwenye jamii hususani wafugaji na wakulima. Uzembe huu umegharimu maisha ya watu wengi ikiwemo kuharibiwa na kuteketewa kwa mali za wananchi huku hatua madhubuti zikishindwa kuchukuliwa kukabiliana na tatizo hilo.

Taifa limeendelea kuwa na mipango ambayo inaendeleza sana Miji na Majiji bila kuwa na mipango ambayo ni shirikishi na endelevu na ambayo inafanya Vijiji kuwa na shughuli za maendeleo na hivyo kupunguza ongezeko la kuhama kutoka Vijijini kuja Mijini.

Wakazi wanaoishi kwenye Miji na Majiji bado wameendelea kukumbwa na kadhia ya bomobomoa katika maeneo ambayo yanadhaniwa kuwa ni utekelezaji wa mipango ya Serikali bila kulipa fidia stahiki kwa mujibu wa sheria; imefika hatua Serikali kubomoa makazi ya watu bila kuzingatia amri ya Mahakama (Rejea Bomoabomoa ya Kimara- Kibamba- Kibaha katika Jiji la Dar es Salaam mwaka 2016/2017)

Makazi ya Miji na Majiji kuendelea kujengwa bila kuzingatia mipango ya mamlaka za Serikali huku taasisi nyingine za Serikali kama vile Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Mamlaka zinazohusika na utoaji wa huduma ya Maji kuendelea kutoa

huduma kwenye maeneo bila kuzingatia kwamba hayapo kwenye mipango miji. Kutokuzingatia mipango kumefanya maeneo ya Miji na Majiji kukabiliwa na mafuriko ya mara kwa mara pamoja na kutokuwepo kwa miundombinu rafiki ambayo husaidia shughuli za uokoaji na kuzima moto wakati wa majanga.

Serikali ya Chadema itafanya mambo yafuatayo;

- a. Serikali ya Chadema itafanya marekebisho makubwa katika sekta ya ardhi ili kumfanya mwananchi kumiliki ardhi pamoja na rasilimali zake za juu na chini ili kumfanya mwananchi kutumia ardhi yake kama dhamana kupata fursa za mikopo. Mpango huo utaenda sambasamba na kuwashirikisha wananchi wenye mahitaji maalum wakiwemo walemavu.
- b. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi na wananchi katika maeneo yao itahakikisha kwamba ardhi yote ya jumla na vijiji kwa hatua za awali inapimwa na kupangwa kwa kutumia teknolojia ili kupunguza migogoro ya ardhi.
- c. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba inaweka mifumo shirikishi ya kutatua migogoro ya ardhi ya Mijini na Vijijini kwa wakati ili kuruhusu shughuli za kiuchumi kufanyika bila vikwazo. Mifumo hiyo itahakikisha kwamba wanawake na walemavu wanashirikishwa kikamilifu.
- d. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itaboresha mipango ya Miji na Majiji ambayo itaboresha makazi na kuboresha ufanisi wa ukusanyaji wa mapato pamoja na kusaidia kuweka na kuboresha miundombinu ya uokoaji na zimamoto wakati wa majanga.
- e. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itaanzisha mpango wa makazi vijijini ikiwa ni pamoja

- na kuhakikisha uwepo wa nyumba bora zenye staha kwa wananchi na kuondokana na nyumba za tembe na nyasi nchini.
- f. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itaboresha huduma za maji, nishati, miundombinu na afya vijijini ili kurahisisha uzalishaji wa bidhaa na huduma na kuchochea maendeleo vijijini.
 - g. Serikali ya Chadema kwa kuzingatia umuhimu wa Jiji la Dar es Salaam itaanzisha Mamlaka ya Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam (Dar es Salaam Metropolitan Council) na kuhuisha muundo wa uongozi na utawala wa usimamizi wa Jiji hilo uliopo sasa ili kuwa na kazi ya kuboresha miundombinu, makazi, huduma za Jamii, mipango Miji pamoja na kuhakikisha biashara na uzalishaji zinafanyika kwa tija na zenye kunufaisha wakazi na wananchi wa Dar es Salaam kwa kuzalisha ajira na kuongeza mapato mara mbili na zaidi kuliko ilivyo sasa.

7.1 MAKAZI NA NYUMBA

Serikali ya Chadema itaunda Mamlaka ya Taifa ya Uendelezaji Makazi na Nyumba (National Housing and Residence Development Authority) itakayofanya kazi iliyokuwa inafanywa na NHC pamoja na kuleta mabadiliko ya makazi ya watu kama ilivyokusudiwa.

Aidha katika kuhakikisha kuwa tunakuwa na makazi na nyumba bora serikali ya CHADEMA itakuwa na *'Mpango wa miaka kumi (2020-2030) wa Uendelezaji wa Nyumba na Makazi ya Taifa (National Housing and Residence Development Plan)'* utalenga kuhakikisha kuwa:

- a. Ujenzi wa nyumba za matope, fito na nyasi unatoweka nchini ifikapo mwaka 2030. Endapo nyumba hizi zitakuwepo, basi zitakuwa kwa ajili ya kumbukumbu ya vizazi vijavyo na kwa dhamira ya kujifunza maisha ya kale yalivyokuwa.
- b. Katika kutimiza adhema na lengo hilo serikali ya CHADEMA itaweka mfumo na utaratibu utakaosimamia na kufidia uvunjaji wa nyumba za zamani (ukiondoa zile ambazo zina umuhimu wa kihistoria, kidini, au uvunjaji wake utaingiliana na mipango mingine) na utafidia kwa kiasi gharama ya ujenzi mpya wa nyumba mpya ili kuhakikisha kuwa wamiliki wanarudi na kumiliki nyumba zao bila madeni makubwa migongoni mwao.
- c. Lengo litakuwa ni kupanua mitaa, kuweka barabara za kisasa, na kupitisha na kufikisha huduma mbalimbali za kijamii. Ili kukidhi adhema hii, serikali ya CHADEMA itahamasisha makampuni makubwa kuingia kwenye biashara ya nyumba na makazi (Real Estate) ambapo wananchi wataundiwa mfumo wa kukopeshwa nyumba (Mortigage System) ili kuwapunguzia adha na suruba za ujenzi. Katika kufanikisha lengo hili, serikali itakuwa mdhamini mkuu.
- d. Kuanzisha mpango wa kuhakikisha kuwa maeneo yote ya makazi nchini yanapimwa, maeneo ambayo hayakupangwa kwa makazi yanahamishwa na maeneo mapya yaliyopangwa yanabuniwa. Nyumba mpya zitajengwa na mamlaka hii kwa ajili ya watu wa kipato cha chini na cha kati katika mfumo na mtindo wenye kuzingatia nafasi, usalama na afya na huduma muhimu za kijamii.
- e. Bajeti ya Serikali ya Taifa itatengwa ili kuhakikisha kuwa kati ya asilimia 8-10 ya bajeti yote ya serikali kila mwaka inatengwa kwa ajili ya kuendeleza makazi na nyumba.
- f. Vifaa vya ujenzi vitatozwa kodi kwa uwiano utakaosaidia kutotofautiana kwa bei kutoka Mkoa mmoja hadi mwingine,

na Wilaya moja hadi nyingine ili kuhakikisha kuwa thamani za nyumba hazitofautiani sana hapa nchini na watu wote wanaweza kumiliki nyumba.

7.2 FURSA YA KUPATA MAJI SAFI NA SALAMA KWA KILA MTANZANIA

Kwa mujibu wa ripoti iliyotolewa kwa ushirikiano wa shirika la afya duniani (WHO) na shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia watoto (UNICEF), mabilioni ya watu duniani wanaendelea kutaabika kutokana na kukosa huduma bora za maji na masuala ya usafi. Maji ndio roho ya uchumi wa dunia, 19% ya matumizi ya maji ni kwa ajili ya viwanda, na 70% zaidi ni katika matumizi ya mnyororo wa uzalishaji kwenye sekta ya kilimo. Pamoja na kujua kuwa Maji ni Uhai, upatikanaji wa maji safi na salama katika sehemu kubwa ya nchi bado ni kitendawili.

Wanawake wamekuwa wahanga wakubwa katika tatizo la upatikanaji wa maji safi na salama. Hii ni kutokana na shughuli nyingi za kifamilia kuhitaji maji kama vile, matumizi ya maji katika uzalishaji na uandaaji wa vyakula, matumizi mahususi ya maji kwenye afya ya uzazi na kadhalika. Wanawake pia ndio wamekuwa wahanga wakubwa kwa matukio ya udhalilishaji na ukatili kama vile ubakaji na kesi nyingine nyingi za kudhuru mwili wanazokumbana nazo wakiwa katika safari za kutafuta maji.

Takwimu zinaonesha kuwa Serikali imekwisha tumia fedha nyingi kutekeleza miradi ya maji katika Programu ya maendeleo ya maji katika awamu ya kwanza (WSDP Phase I (2007-2015) na awamu ya pili inayoishia mwaka 2021, fedha zilizo tumika ni takribani dola za kimarekani bilioni 3.33 ambazo ni sawa na shilingi trilioni 6.9. Mbali na uwekezaji wote huo kwenye maji lakini tatizo la maji limeendelea kuwa sugu katika maeneo mengi ya nchi yetu.

Serikali ya CHADEMA itafanya yafuatayo kuondokana na matatizo kwenye sekta maji;

- a. Serikali ya Chadema itaunda Wizara Maalumu ya Kudumu ya Maji ambayo itatengewa bajeti ya kutosha kwa ajili ya kuendeleza na kuimarisha sekta ya maji kwa kushirikiana Sekta binafsi na halmashauri za wilaya na miji.
- b. Itahakikisha kuwa utekelezaji wa miradi ya maji utakuwa shirikishi na wa uwazi ili wanufaikaji nao kwa nafasi zao wawe ni washiriki na wasimamizi wa miradi husika.
- c. Kutakuwa na mipango ya utandazaji mabomba ya maji ya kisasa katika halmashauri zote nchini ili kuhakikisha kiasi kikubwa zaidi cha maji kinawafikia wananchi kutoka vyanzo vyake na siyo kupotea njiani kutokana na miundombinu mibovu.
- d. Kutoa elimu kwa wananchi ikilenga kutunza vyanzo vya maji na mazingira kwa ujumla kwa kutilia maanani kuwa maji ni sehemu ya usalama wa taifa.
- e. Kuhakikisha kuwa ardhi oevu (wetlands) inalindwa kwa ajili ya matumizi ya kizazi hiki na kijacho kwa nguvu zote kwa kuzingatia ushauri wa wataalamu.
- f. Huduma za maji vijijini na mijini zitatozwa viwango tofauti ili kuhakikisha kwamba wale wanaoishi na kufanya kazi kwenye mazingira mazuri ya kujiongezea kipato mijini wanachangia upatikanaji wa huduma hizo kwa wale wanaoishi kwenye myazingara magumu ya huko vijijini.
- g. Halmashauri kuingia ubia na Sekta binafsi kwa mfumo wa PPP katika kutoa huduma za maji ya uhakika kwa wananchi ikiwa ni katika kupambana na uwezo mdogo kifedha wa halmashauri zetu na hivyo kutoa huduma hiyo.

- h. Kuweka mfumo madhubuti wa kudhibiti maji taka katika miji na maeneo yote ya makazi ya watu ili kuhakikisha kuwa majitaka hayasababishi kusambaa kwa magonjwa mbalimbali
- i. Kuweka mfumo wa kuvuna maji ya mvua katika maeneo yote nchini, hili litafanywa kwa kushirikiana na sekta binafsi, ili kuhakikisha kuwa maji ya mvua hayapotei bure na badala yake yanahifadhiwa kwa ajili ya matumizi ya binadamu na wanyama.

8. KUJENGA KILIMO,UVUVI NA UFUGAJI .



Kilimo ndiyo msingi mkuu wa maendeleo ya uchumi wa Tanzania. Kilimo ni chanzo kikuu cha ajira kwa zaidi ya 80% ya nguvu kazi ya Taifa. Sekta ya Kilimo na ufugaji inakabiliwa na changamoto mbalimbali lakini kubwa ni kukosekana kwa soko na gharama kubwa za maandalizi na uvunaji wa mazao na mifugo.

Aidha, Wakulima wamekua wakiuza mazao yao kwa wachuuzi wa mazao na mifugo bila kusindika jambo ambalo linafanya thamani ya mazao hayo na mifugo kwa ujumla kuwa chini. Miundombinu mibovu katika maeneo ya kilimo pamoja na ukosefu wa kusindika mazao ya mifugo na kilimo unachangia pia kukosekana kwa tija kwenye mazao ya kilimo na mifugo.

Kwa kuwa sekta ya kilimo inaendelea kuwa ndio chanzo kikuu cha uhakika cha kipato na ajira kwa Watanzania walio wengi, ni kusudio la serikali ya Chadema kuiimarisha na kuwa bora zaidi kuliko wakati mwingine wowote.

Chadema inatambua kuwa mahitaji makuu kwenye kilimo hapa nchini kwetu ni pamoja na :

- Soko la mazao ya kilimo kwa kuimarisha ushirika
- Pembejeo za kilimo kwa serikali kuweka ruzuku
- Ukuzaji wa teknolojia ya kilimo
- Kuongeza thamani kwenye mazao
- Uhifadhi wa mazao (storage)

Sekta ya uvuvi inakabiliwa na changamoto mbalimbali kama vile kukosekana kwa nyenzo za kuvulia samaki, wavuvi kuchomewa nyavu zao ambazo zimezalishwa na viwanda vya ndani na kuhakikiwa na TBS, kutaifishwa kwa boti za uvuvi, kuvamiwa na maharamia na tozo mbalimbali wanazotakiwa kulipia .

Aidha sekta hii inakabiliwa na changamoto ya kukosekana kwa njia za kisasa za kuhifadhi mazao ya samaki, mitaji na masoko ya uhakika .

Sekta ya mifugo ina changamoto kubwa hasa ya kukosekana sehemu maalum za malisho na maji kwa ajili ya mifugo na hivyo kuwafanya wafugaji kuhamahama na au kufukuzwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Ukosefu wa viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo ili kuyaongezea dhamani, kukosekana kwa huduma za ugani, gharama kubwa za madawa ya mifugo, uhaba wa wataalamu wa mifugo na kukosekana kwa masoko ya uhakika ya ndani kwa ajili ya bidhaa za mifugo.

Wafugaji wanakabiliwa na tozo nyingi wakati wa kuuza mifugo yao kwani wanatakiwa kulipia vibali mbalimbali kabla ya kuuza na au kusafirisha mifugo yao.

Pamoja na utajiri mkubwa wa sekta ya mifugo wafugaji hawakopesheki kwenye sekta za fedha kwani mifugo haitambuliki kama dhamana na hivyo kuwafanya wafugaji kushindwa kujiendeleza .

Serikali ya CHADEMA itafanya yafuatayo ili kuboresha sekta ya kilimo;

Lengo kuu la kukuza sekta ya kilimo ni kuwa na chakula cha kutosha na kukabiliana na lishe duni pamoja na kuhakikisha kuwa kilimo kinaleta tija kibiashara na hivyo kuchangia katika kuongeza pato la taifa.

Serikali ya Chadema itaimarisha teknolojia ya kilimo ili kukuza uzalishaji na kuongeza thamani ya mazao.

- a. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itahakikisha kwamba inaweka mkakati wa muda mfupi kwa ajili ya uzalishaji, uhifadhi, usambazaji na soko la kutabirika la mazao ya wakulima nchini.
- b. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itahakikisha kwamba inaongeza viwanda vya usindikaji wa mazao na kupunguza tatizo la kuuza bidhaa ghafi.
- c. Serikali ya Chadema itatoa msukumo maalum kwa taasisi za utafiti wa Samaki ili kupata mbegu bora zinazohimili mazingira nje ya maziwa na bahari, kwa ajili ya ufugaji wa samaki (*fish farming/aquaculture*) wenye tija kwa wananchi na kukuza uchumi.
- d. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba kunakuwa na mkakati endelevu wa hifadhi ya chakula ili kuhakikisha kwamba kunakuwa na chakula cha kutosha kukabiliana na dharura mbalimbali wakati wa majanga.
- e. Serikali ya Chadema itahimiza ufugaji wa kitamaduni lakini pia itahakikisha kwamba inatoa elimu ya ufugaji wenye tija kibiashara kwa wafugaji ili kukuza mapato kwa wakulima.
- f. Serikali ya Chadema itaweka utaratibu wa bima kwa wakulima na wafugaji ili kupata fidia wakati wa majanga au ukame.
- g. Itaimarisha na kuboresha soko la ndani ili kukabiliana

na anguko la bei ya mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji, hii itasaidia kulipa gharama za uzalishaji na kupata faida kutokana na kuuza mazao yao.

- h. Serikali ya Chadema itaimarisha uchakataji (processing) wa mazao ya kilimo, uvuvi na ufugaji ili kuongeza thamani na bidhaa zetu kuwa shindani kwenye soko la nje.
- i. Kuunda vyama vya ushirika, kusimamiwa na kuendeshwa kwa ridhaa ya wanaushirika wenyewe ili kuwezesha shughuli za kilimo, uvuvi na wafugaji wenye tija kiuchumi.
- j. Kusimamia bei za mazao na ruzuku zingine badala ya ruzuku kwenye pembejeo pekee.
- k. Serikali ya Chadema itahimiza matumizi ya mbolea za asili kama vile samadi na mboji katika maeneo ambayo mazao yanastawi kwa matumizi ya asili ya ardhi.
- l. Serikali ya Chadema itaanzisha ushirikiano na taasisi za kimataifa za kilimo cha kioganiki. Maeneo maalumu yatatengwa ili kuwe na sehemu ambazo zitatumika kuanzisha kilimo kikubwa cha kioganiki.
- m. Itaanzisha Vyu vya ufundi na Shule za Sekondari za Kilimo zitatumika katika kutoa mafunzo ya kilimo cha oganiki kama sehemu ya kuwaandaa wanafunzi katika maisha ya kilimo cha kisasa. Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine Morogoro kitatakiwa kuandaa mtaala ambao utaingiza mafunzo ya kilimo cha oganiki na kufanya utafiti katika mazingira ya Tanzania.
- n. Serikali ya Chadema itapitia upya mikataba yote mikubwa ya kilimo ambayo Serikali imeingia na taasisi au nchi za nje ili kuweza kuhakikisha kuwa maslahi ya nchi na mahitaji ya chakula yanazingatiwa. Hii itakuwa ni pamoja na kulinda usalama wa chakula nchini.

- o. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itaweka mkazo wa kukuza mazao mbalimbali ya nafaka kama ngano na shayiri kwa kuweka utaratibu utakaofufua mashamba makubwa ya mazao hayo nchini ili yaweze kuzalisha kama ilivyokuwa hapo awali.
- p. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itahakisha kuwa taasisi au mataifa ya nje yanayotaka kuwekeza katika kilimo nchini yanafanya hivyo kwa kuingia mikataba na vijiji na maeneo husika ili kuhakikisha kuwa wananchi wanaoishi katika maeneo husika wananufaika na uwekezaji mkubwa wa kilimo kiteknolojia na kimasoko.
- q. Serikali ya Chadema itaweka msukumo wa kipekee kwa Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine na vyuo vingine vya kilimo ili viwe ni vituo vya utafiti kwa vitendo katika mazao, mifugo na chimbuko la mbegu bora . Lengo ni kuhakikisha kuwa nchi inajitosheleza katika mahitaji ya mbegu na kuliondolea taifa aibu ya kuagiza mbegu bora za kutoka nje ya nchi.
- r. Serikali ya Chadema itahamasisha uanzishwaji wa kilimo cha mijini (urban farming) hasa katika mazao ya bustani za mboga na matunda. Lengo ni kuhakikisha kuwa katika miji yote mazao kama mboga na matunda yanapatikana kwa urahisi, katika mazingira safi na salama. Hii itakuwa ni pamoja na kuweka mfumo wa kuanzisha viwanda vidogovidogo vya kuhifadhia matunda na mboga.
- s. Uwekezaji mkubwa wa uhifadhi wa matunda na mboga utawekewa utaratibu kwa kuweka unafuu wa kodi kwa makampuni yatakayoanzisha viwanda vya kusindika matunda na mboga.
- t. Serikali ya Chadema itahimiza ufugaji bora ili mfugaji aweze kupata faida kutokana na ufugaji wake. Itahimiza uanzishwaji wa ushirika wa masoko (marketing

- cooperatives) ili wafugaji waweze kuwa na nguvu katika kuuza mazao yatokanayo na ufugaji.
- u. Serikali ya Chadema itaainisha maeneo ya kiuchumi yatakayosaidia Taifa kuwa la wazalishaji kwa kujenga viwanda katika miji husika ili kuchakata mazao mbalimbali ya kilimo, uvuvi na mifugo; kuleta teknolojia katika taifa na kuhakikisha kuwa kilimo, uvuvi na ufugaji ni moja ya “viwanda” vikubwa vya uzalishaji wa uchumi imara.
 - v. Serikali ya Chadema itawekeza katika kutengeneza barabara zinazounganisha kata na kata, wilaya na wilaya na mikoa na mikoa ili kurahisisha usafirishaji wa mazao kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Katika kuimarisha miundombinu ya uchukuzi, mpango wa muda mrefu wa serikali ya Chadema ni kuunganisha kila mkoa na njia ya reli ili kuweza kusafirisha mizigo mikubwa zaidi, kwa haraka na kwa uhakika zaidi.
 - w. Serikali ya Chadema itawekeza katika teknolojia ya kuvuna maji ya mvua, mabwawa, mito na maziwa ili kukuza kilimo cha umwagiliaji na pia kuwa na malambo kwa ajili ya matumizi ya mifugo.
 - x. Ili kutekeleza mipango ya kilimo ya muda mrefu, Serikali ya Chadema itaunda mamlaka inayojitegemea kwa ajili ya Kilimo (Tanzania Agricultural Authority).
 - y. Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa NARCO – Shirika la Ranchi la Taifa linaingia kwenye ushindani wa kibiashara katika uzalishaji wa nyama na chakula nchini.
 - z. Mradi wa kuunganisha taasisi zote za utafiti wa kilimo na mifugo nchini kwa kutumia intaneti utatekelezwa ili ifikapo 2023 taasisi zote hizo ziwe katika mtandao wa kisasa wa mawasiliano.

8.1 UVUVI WA BAHARI KUU (DEEP SEA FISHING)

Jamhuri ya Muungano ina eneo la ukanda wa pwani (territorial sea) la kilomita za mraba 64,000 pamoja na eneo maalum la kiuchumi la Bahari Kuu (Exclusive Economic Zone-EEZ) kilomita za mraba 223,000 ambalo ni sawa na asilimia 24% ya eneo lake la ardhi. Aidha, Jamhuri ya Muungano ina eneo la madini ya chini ya bahari (extended continental) kilomita za mraba 17,900 na eneo la pwani (coastline) la kilomita 1,400.



Jamhuri ya Muungano imeridhia Mkataba wa Kimataifa juu ya Sheria za bahari (UNCLOS) wa mwaka 1982 ambao unaipa Mamlaka ya kusimamia na kudhibiti rasilimali zinazopatikana eneo la chini ya bahari (jurisdiction over the exploration and exploitation of marine resources in its adjacent section of the continental shelf), eneo ambalo linaweza kuongezwa hadi maili 200 kutoka eneo la ukanda wa pwani .

Aidha, Jamhuri ya Muungano imeridhia mkataba juu ya utekelezaji (Compliance Agreement) wa mwaka 1993 sambamba na mikataba mengine inayohusu masuala ya Uvuvi wa Bahari Kuuna rasilimali zinazopatikana chini ya bahari.

Kwa mujibu wa utafiti wa Jarida la sayansi la uchumi wa uvuvi wa bahari kuu (Science Journal on The Economics of fishing the high seas, 2018), inaonyesha kwamba jumla ya samaki waliopatikana bahari kuu mwaka 2014 walikuwa ni tani milioni 4.4 (4.4 milion metric tons) ambao uliingiza jumla ya mapato yatokanayo na kodi kiasi cha Dola bilioni 7.6.

Vile vile, upatikanaji wa samaki ulikuwa kwa asilimia 17% kutoka 2007 hadi 2011 na kufikia jumla ya tani milino 7.2 hadi mwaka 2014 mashariki mwa bahari ya hindi pekee (FAO, 2014). Aidha, Ukanda wa bahari ya hindi unatoa asilimia 19% ya samaki aina ya jodari (tuna) duniani ambao ni sawa na milioni 1.7, na hii ni muhimu kwa ajili ya chakula, ajira na mapato ya kodi (revenues) kwa nchi zenye bahari (coastal states) ambapo asilimia 84% ni samaki wa jamii tuna kutoka bahari Kuu (Indian Tuna Commission - IOTC).

Takwimu za hali ya uchumi za mwaka 2017 zinaonesha kuwa, mapato yaliyotokana na shughuli za uvuvi hapa nchini huchangia 2.2 % ya pato ghafi la Taifa (GDP), na tasnia nzima ya uvuvi inachangia 10 % ya mauzo nje ya nchi (Annual fisheries statistics report 2014).

Aidha, kwa mujibu wa tafiti, takriban asilimia 77% ya meli zinashughulika na uvuvi wa bahari kuu (ABNJ) duniani ni meli zinazomilikiwa na Nchi za China, Taiwan, Japan, Indonesia, Spain na Korea Kusini.

Pamoja na Jamhuri ya Muungano kuwa na eneo kubwa la ukanda wa pwani na eneo la bahari maalum la kiuchumi la Bahari Kuu. Na pamoja na ukweli kwamba eneo letu lina kina kikubwa na samaki wengi, na kwamba tumeshindwa kuwa na bandari mahususi za uvuvi, na viwanda vikubwa vya samaki kwa ajili ya biashara nchini na soko la kimataifa.

Aidha, nchi yetu hainufaiki ipasavyo na rasilimali hiyo na badala yake meli za kigeni hufika na kuwavua samaki hao, wengi wakiwa wa aina ya Jodari, samaki wenye gharama kubwa katika masoko ya kimataifa.

Vile vile, pamoja na Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu (DSFA) kuanzishwa mwaka 2010 iliyopewa majukumu pamoja na mambo mengine kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu, kutoa leseni kwa ajili ya uvuvi wa bahari kuu na kuzikagua meli hizo, bado kumeendelea kuwepo tatizo kubwa katika uvuvi wa Bahari Kuu.

Kwa kuwa Chadema inatambua kuwa uvuvi wa bahari kuu ni suala la ushirika baina na Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, hivyo kabla ya kufanya yafuatayo itatulazimu kukaa na kukubalina na mshirika wetu wa Muungano;

- a. Serikali ya Chadema itaanzisha mchakato wa kuridhia Mkataba wa kazi za Uvuvi (The Work in Fishing Convention, 2007 – No. 88), *Port State Measure Agreement (PSMA)* na *UN Fish stock Agreement*.
- b. Serikali ya Chadema itaimarisha ushirikiano na Taasisi za uvuvi za kikanda na zile zilizopo katika bahari ya hindi magharibi (Western Indian Ocean-WIO) ili kuweza kubadilishana taarifa kuhusiana na mambo mbali mbali ikiwemo uvuvi haramu (IUU fishing) na samaki wanaohamama kama samaki aina ya jodari (Tuna) na aina yake kwa Ukanda wetu wa EEZ.
- c. Serikali ya Chadema itapitia na kuandaa Mkakati wa Kufuatilia, kudhibiti na kuchunguza (Monitoring control and surveillance –MCS) na itifaki zinazokwenda sambamba na sheria za kimataifa na kikanda juu ya uvuvi haramu wa bahari kuu.
- d. Serikali ya Chadema itaandaa Mpango Kazi utakaoruhusu usajili wa meli za uvuvi za kimataifa kwa kutumia mfumo maalum wa utambuzi wa meli (Unique Vessel Identifier –

- UVI) kupitia IMO. Mamlaka za Uvuvi kwa kushirikiana na Mamlaka za Usafiri wa bahari zitaandaa mfumo huu na itifaki husika au Hati ya makubaliano (MoU)
- e. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itanunua Boti kubwa ya kisasa itakayoweza kufanyakazi za doria na utafiti kwenye ukanda wote wa bahari kuu ili kukabiliana na ujangili wa Meli za nje kuvua na kuipotezea serikali mapato yake .

9. MAZINGIRA, MABADILIKO YA TABIA NCHI NA NAMNA YA KUKABILIANA NA MAJANGA

9.1 MAZINGIRA

Chadema inaamini kuwa mazingira hujumuisha vitu vyote vinavyounganisha ardhi, hewa, anga, maji, bio-anwai, misitu, wanyamapori, madini na miundo mfumo wa ikolojia kwa ujumla wake. Nchi yetu kwa sehemu kubwa imejaaliwa kuwa na mazingira ya asili na mandhari ya kuvutia katika maeneo ya bahari, maziwa, ardhi na milima. Si ajabu kuwa maswala ya mazingira yatajitokeza katika sehemu ya maswala ya sekta za maliasili, utalii, kilimo, ufugaji, uvuvi, makazi, uchimbaji madini na aina ya nishati binadamu anayochagua kutumia katika kujiletea maendeleo.

Sehemu hii ya ilani inaweka msisitizo katika tafsiri ya mazingira kama inavyojitokeza katika eneo la mabadiliko ya tabia nchi na swala la namna ya kukabiliana na majanga.

9.2 MABADILIKO YA TABIANCHI

Chadema inaelewa kuwa mabadiliko ya tabia nchi ni hali inayotokana na mabadiliko ya hali ya hewa ambayo hupimwa kwa kuangalia iwango cha joto, mvua na nguvu ya upepo ambayo imekuwepo kwa muda mrefu na mara nyingi huwa ni kuanzia miaka kumi na kuendelea.

Chadema inatambua mabadiliko ya tabia nchi hutokea kwa kusababishwa na utoaji wa hewa ukaa inayotokana na mabaki ya viumbe hai, matumizi ya ardhi na masuala mtambuka. Mabadiliko ya tabia nchi huathiri kila mahali katika dunia tunayoishi. Kama Taifa, tumeshuhudia athari za mabadiliko ya tabia nchi kama vile ukame wa mara kwa mara na mvua kubwa za muda mrefu. Mabadiliko hayo huathiri shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, uchukuzi, nishati, biashara na shughuli nyingine za kijamii na kiuchumi. Chadema itahimiza ushirikishwajiwa jamii kwa kuwajengea uelewa na

kuwahamasisha juu ya namna ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi.

Serikali ya Chadema itatengeneza sera na mkakati shirikishi katika sekta zote juu ya namna ya kukabiliana na changamoto za mabadiliko ya tabia nchi. Lengo la sera hii ni kuhakikisha inaboresha maisha ya Watanzania kwa kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi za sasa na za baadaye kwa kuwa na njia za kupunguza athari hizo pamoja na kupunguza shughuli zinazosababisha kutokea kwa mabadiliko ya tabia nchi.

Serikali ya Chadema itatekeleza yafuatayo katika eneo hili:

- a. Itasisitiza matumizi kidogo ya nishati zinazosababisha hewa ukaa kwa ajili ya kuwa na nishati isiyokuwa na athari za kimazingira.
- b. Itawekeza kimkakati katika miradi ya kupunguza athari za tabia nchi kwa kufanya tafiti za mimea na mbegu kwa ajili ya kuzalisha chakula na kulinda ikolojia.
- c. Itaweka mkazo kwenye matumizi endelevu ya ardhi kama vile maji, mimea, wanyama kwa ajili ya kupata mahitaji ya binadamu kwa ajili ya maendeleo ya baadaye .
- d. Itahakikisha kuwepo kwa miradi ya upandaji miti kwa ajili ya kupunguza athari za hewa ukaa na pia itahamasisha na kuwajengea uelewa wananchi katika maeneo yao kuhusu namna ya kupunguza na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi.
- e. Itanzisha mfuko maalum wa mabadiliko ya tabia nchi kwa ajili tafiti, usimamizi na tathmini kuhusu mabadiliko ya tabia nchi.
- f. Itaunga mkono juhudi za kimataifa za kupunguza hewa ukaa.

Katika kutekeleza sera na hatua mbalimbali katika eneo hili serikali ya Chadema italenga:

- a. Kuwajengea wananchi uwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi, jambo ambalo litaboresha maisha yao.
- b. Kuwaongezea wananchi uelewa wa athari za mabadiliko ya tabia nchi katika maisha yao ya kila siku na hivyo kuchukua tahadhari.
- c. Kusimamia kuongezeka kwa miundombinu ya kuzuia athari za mabadiliko ya tabia nchi na hivyo kunusuru mali na maisha ya wananchi.
- d. Kusimamia kuwepo uwekezaji wa kuridhisha kwenye miradi ya kimkakati ya nishati jadidifu itasaidia kupanua fursa za uwekezaji ambapo pato la Taifa litaongezeka, mazingira yatatunzwa na fursa za ajira zitaongezeka.

Serikali ya Chadema itaweka mkazo kisera na kiutendaji ufuatiliaji wa karibu wa yafuatayo:

- a. Uwepo wa Sera ya Mabadiliko ya Tabia Nchi
- b. Kuchukuliwa hatua kuhakikisha kuwa zipo njia za kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi (kupunguza vyanzo vya hewa ukaa)
- c. Kuchukuliwa hatua za kupunguza athari za mabadiliko ya tabia nchi
- d. Uanzishwaji mfuko maalum wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia nchi
- e. Kuchukuliwa hatua kuimiza ushirikishwaji jamii katika kukabiliana na mabadiliko ya tabia nchi

9.3 KUKABILIANA NA MAJANGA

Masuala ya mabadiliko ya tabia nchi ni mambo ambayo yamevuta mijadala ya ndani na kimataifa na hivyo kupelekea haja ya kuwa

na mipango ya muda mfupi na muda mrefu ili kukabiliana na athari za kimazingira pamoja na kuhimili majanga mbalimbali kama vile ukame wa muda mrefu ambao husababisha njaa, mvua kubwa na mafuriko yasiyotarajiwa, magonjwa ya mlipuko na athari kwenye uoto wa asili.

Aidha, mvua kubwa ambazo kwa muda mrefu zimekua zikinyesha maeneo mbalimbali nchini na kupelekea mafuriko katika nyanda za kusini, kanda ya Ziwa, Kanda ya Kati katika Mkoa wa Morogoro na mwanzo mwa mwaka huu katika Mkoa wa Kilimanjaro; zimeonyesha ni jinsi gani Serikali ya Chama cha Mapinduzi isivyokua na mipango, bajeti pamoja na mifumo thabiti wa kukabiliana na maafa.

Hivyo basi, uongozi mpya wa Serikali ya Chadema unanuia kuachana na tabia ya mazoea ambayo imepelekea kutolewa kauli tata kutoka kwa viongozi mathalani kauli ya “Serikali haijaleta tetemeko” na badala yake Serikali ya Chadema itakua mfariji Mkuu wa watu wake kwa vitendo kwa kufanya yafuatayo;

- a. Serikali ya Chadema itaanzisha wakala wa kukabiliana na majanga. Wakala huyu atakuwa na wajibu wa kuunganisha taasisi zote ambazo zinahusika kwa njia moja ama nyingine na majanga.
- b. Serikali ya Chadema itatenga kwenye bajeti fedha za ndani kwa ajili ya kukabiliana na majanga ikiwa ni pamoja na kuwasaidia kwa wakati wananchi walioathirika na majanga mbalimbali.
- c. Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa Halmashauri zote nchini zinakuwa na kitengo maalum cha kukabiliana na maafa chenye bajeti toshelevu.
- d. Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa kuna nyenzo na vifaa vya kisasa kwa ajili ya uokoaji pindi yanapotokea majanga mbalimbali kama vile moto, mafuriko, matetemeko na mengineyo.

10.0 MIUNDOMBINU: UCHUKUZI, MAWASILIANO NA TEHAMA

Miundombinu inajumuisha uwepo wa nyenzo na mifumo ambayo huwezesha watu kufanya kazi zao, mathalani miundombinu ya teknolojia ya habari na mawasiliano, nishati, uchukuzi, huduma za posta na usimamizi wa maji safi na mifumo ya maji taka. Nchi itapiga hatua kimaendeleo kama Serikali itasimamia na kuendesha miundombinu vizuri. Mipango na maamuzi yote yanayofanyika yanatakiwa yaende sambamba na uwepo wa miundombinu kwa ajili ya utekelezwaji wake. Licha ya kuwa na mahitaji makubwa ya fedha, miundombinu ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya uchumi na ustawi wa Taifa. Kwa hiyo, uamuzi wa kupanga na kuweka miundombinu ni lazima iwe shirikishi na kuzingatia idadi na mahitaji ya watu ya muda mrefu, mazingira na maendeleo endelevu ya kiuchumi na kijamii.

Serikali iliyo madarakani imejinasibu na ujenzi wa miradi mikubwa katika sekta ya Miundombinu kama ujenzi wa barabara, reli ya kisasa, ununuzi wa ndege, na utengenezaji wa meli za kusafirisha abiri wengi na mizigo mikubwa katika maziwa yaliyo ndani ya nchi na mipakani mwa nchi pamoja katika bahari ya Hindi inayopakana na Tanzania.

Chadema inaelewa na kutambua kuwa miradi ya miundombinu inagharimu fedha nyingi na masuala mengi yanayoambatana nayo ambayo inabidi yashughulikiwe na kusimamiwa. Chadema inatambua kuwa ugharamiaji wa miundombinu hauwezi kufanywa na Serikali pekee kwa kuwa kwa kufanya hivyo Serikali itashindwa kugharamia huduma nyingine za kijamii. Hivyo, Chadema itaanzisha mfumo wa kugharamia miundombinu kwa kutumia sekta binafsi ambao utakuwa wa gharama nafuu.

Chadema inaunga mkono mfumo wa ugharamiaji wa miundombinu kwa kutumia kodi, mikopo na misaada kutoka nje ya nchi. Hii itahusisha mfumo wa ugharamiaji kwa pamoja kati ya

Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Chadema itahimiza ushiriki imara wa sekta binafsi katika kuwekeza kwenye miradi ya miundombinu kwa kutumia ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi kwa utaratibu kwamba sekta binafsi inajenga na kuendesha miundombinu na baadaye kuhamishia umiliki kwa Serikali.

Serikali ya Chadema itahimiza ushiriki wa wawekezaji wa ndani na wa nje katika miradi ya ujenzi wa miundombinu. Chadema itahimiza ushiriki wa Mashirika ya Umma katika ujenzi wa miundombinu.

Serikali ya Chadema itaweka utaratibu wa kisera na kisheria ili kuwezesha kuwa na mbinu za kugharamia ujenzi wa miundombinu ambao utakuwa na uhakika na dhamana kwa uwekezaji uliofanyika ikiwemo kuweka utaratibu wa kuepuka hasara inayoweza kutokea kutokana na mabadiliko ya kisiasa. Utaratibu wa kisera utahakikisha unamlinda mtumiaji wa miundombinu dhidi ya hujuma zozote au kukataliwa kutumia miundombinu husika.

Kwa ujumla, Serikali ya Chadema itachukua hatua zifuatazo;

- a. Serikali ya Chadema itachukua hatua za kuboresha mfumo wa ugharamiaji wa ujenzi wa miundombinu ikiwa ni pamoja na kuimiza kuwepo ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi katika ugharamiaji wa ujenzi wa miundombinu.
- b. Serikali ya Chadema itahimiza ushiriki wa sekta binafsi katika mfumo wa Jenga, Endeleza na Hamisha (Build, Operate and Transfer)
- c. Serikali ya Chadema itapitisha utaratibu wa Kisera na Kisheria kuwezesha mfumo wa kugharamia ujenzi na undeshaji wa miundombinu kuanza kutumika.

10.2 UCHUKUZI: USAFIRI WA NCHI KAVU, USAFIRI WA MAJI, USAFIRI WA ANGA.

Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa nchi imeunganishwa na mtandao wa barabara bora na zenye usalama kwa watumiaji. Mtandao huo utajengwa kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi ili kurahisisha huduma za usafiri nchini.

Chadema itaboresha na kupanua mtandao wa reli kwa ajili ya abiria na mizigo hapa nchini na kuunganisha mtandao huo katika nchi zinazopakana na Tanzania. Aidha, Chadema itahakikisha kuwa mtandao wa reli unaunganishwa na bandari pamoja na viwanja vya ndege vya kimataifa.

Serikali ya Chadema itaboresha vituo vyote vya reli ili kukidhi mahitaji ya usafiri wa reli. Pia inalenga kuwa na treni za kisasa za mwendo kasi kurahisisha usafiri wa reli nchini. Chadema inatambua kuwa usafiri wa majini ni kichocheo cha biashara, burudani na ni eneo la kimkakati la ulinzi na usalama. Chadema itahakikisha kuwa inajenga na kuboresha bandari kwa ajili ya mashua za watu binafsi na kuweka mazingira mazuri ya kuwa na meli za Watalii.

Serikali ya Chadema itahimiza ushiriki wa sekta binafsi kwa kuyavutia mashirika makubwa ya meli kuja kuwekeza nchini. Chadema itahakikisha kuwa inazingatia vigezo vyote vya ulinzi na usalama katika mfumo mzima wa usafiri Baharini. Serikali ya Chadema itaboresha na kuendeleza vivuko vyote kwa ajili ya kuwaunganisha wananchi.

Chadema inakusudia kujenga na kuboresha mtandao wa mabomba ya mafuta na gesi na kuunganisha na Makao Makuu ya Kanda zote kwa kuzingatia vigezo vya kibiashara na faida. Hii itajumuisha ujenzi wa vituo vya gesi na mafuta bandarini na kwenye Kanda mbalimbali kwa kuzingatia vigezo vya kiusalama. Chadema

inakusudia kuanzisha mfumo wa usafiri wa anga wenye ufanisi, unaozingatia ubora na wenye gharama nafuu.

Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa Mikoa yote inapata huduma za kibishara za usafiri wa anga. Aidha, Chadema itahakikisha kwamba Tanzania inakuwa na Shirika la Ndege ambalo litamilikiwa kwa ubia kati ya sekta binafsi na Serikali, litakaloendeshwa kibiashara kwa kuzingatia nguvu ya soko na litakalotoa huduma za usafiri za ndani na kimataifa. Hii itajumuisha ujenzi na uboreshaji wa Viwanja vya Ndege kwa viwango na ubora wa kimataifa ili kukidhi mahitaji ya sekta ya usafiri wa anga.

Katika kutekeleza sera zake katika eneo hili la miundombinu serikali ya Chadema itakuwa na lengo la kuwanufaisha wananchi kwa kuchukua hatua stahiki kama ifuatavyo:

- a. Kwa kushirikiana na sekta binafsi serikali ya Chadema itaboresha miundombinu ili kupunguza gharama za kufanya shughuli za kibiashara na kupunguza muda mrefu wa kusafiri na kusafirisha mizigo. Aidha, maboresho haya yatasaidia katika kuwepo usalama zaidi kwa watumiaji wa vyombo vya usafiri, itapunguza idadi ya vifo, majeruhi na hasara zinazotokana na ajali za barabarani.
- b. Serikali ya chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itahakikisha kuwa huduma zinazotolewa kwenye viwanja vya ndege, Bandari na vituo vya reli zinakuwa za viwango vya kimataifa.
- c. Mfumo wa uchukuzi ulioboreshwa utaongeza ajira zenye kipato na pia kuboresha sekta nyingine zinazoambatana kama vile hoteli, utalii, ujenzi na shughuli nyingine mbalimbali za kiuchumi na kijamii.
- d. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itaboresha viwanja vya ndege na kuweka maeneo maalum ya kuhifadhi mazao ya mifugo, uvuvi na kilimo kama vile

mbogamboga, parachichi na maua kwa ajili ya kusafirisha kwenda nje ya Nchi (Cooling system).

- e. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itahakikisha kuwa zinapatikana meli na boti za kisasa kwa ajili ya usafirishaji wa abiria, mizigo na watalii. Aidha zitakuwepo meli na boti kwa ajili ya uokoaji kwenye bahari na Maziwa.

10.3 TEKNOLOJIA YA HABARI NA MAWASILIANO (TEHAMA)

Chadema inatambua kuwa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni msingi wa kuwa na jamii imara yenye maarifa na uchumi endelevu kwa mustakabali wa nchi. Chadema itawekeza kwenye teknolojia ya habari, kuwa na mfumo wa Satelaiti na kuboresha usalama wa mtandao wake ili kuendana na ukuaji wa teknolojia hiyo duniani.

Chadema inaamini katika uhuru wa matumizi ya mtandao katika kukua na kustawi kiuchumi na kijamii

Chadema inahimiza uhuru wa kuwa na mtandao wa mawasiliano kwa wananchi wote. Chadema inachukulia teknolojia ya habari kuwa ni nyenzo muhimu katika maarifa ya kijamii na si vinginevyo.

Chadema itahakikisha usalama wa mtandao kwa watumiaji wote na pia itahakikisha kuwa kuna faragha kwa watumiaji pamoja na kuhakikisha kuwa watumiaji hawashambuliwi wala kunyanyaswa kwa namna yoyote ile.

Chadema itawekeza kwenye teknolojia ya Satelaiti ili kuwezesha shughuli za kimtandao za Serikali pamoja na kutumia teknolojia hiyo kwenye kilimo, biashara, uwekezaji, kufuatilia hali ya hewa na mabadiliko ya tabia nchi, matumizi ya ardhi pamoja na kukabiliana na majanga mbalimbali.

Chadema itatumia teknolojia ya habari na mawasiliano katika masuala ya kijamii na pia katika masuala ya kijeshi. Chadema inaamini katika ushirikiano na mataifa mengine katika kutafuta suluhu na changamoto za kimawasiliano.

Katika kutekeleza sera zake katika eneo hili la TEHAMA serikali ya Chadema itakuwa na lengo la kuwanufaisha wananchi kuchukua kila hatua stahiki kuhakikisha kuwa :

- a. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itahakikisha kuwa Watanzania watakuwa na uhakika wa kupata taarifa na kupanua wigo wa mawasiliano kwa kuboresha miundombinu ya TEHAMA.
- b. Serikali ya Chadema itaweka sera na sheria zinazohakikisha kuwa Wananchi watakuwa salama wakati wa kutumia mtandao na pia watahakikishiwa faragha na kutoingiliwa kimtandao na watu wengine, wala kubughudhiwa kwa namna yoyote ile.
- c. Jamii itapata taarifa za biashara, kilimo pamoja na taarifa za hali ya hewa na hivyo kuweza kujipanga kukabiliana na majanga mbalimbali.
- d. Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa Jamii itapata taarifa kirahisi pamoja na kufanya miamala ya kifedha na kibiashara kwa urahisi.
- e. Serikali ya Chadema ikishirikiana na sekta binafsi itahakikisha kuwa gharama za mawasiliano zinapungua ili kumwezesha kila mwananchi kuzimudu.
- f. Serikali ya Chadema itasimamia na kuhakikisha kuwa kanzi data iko salama na inatumika kwa malengo yaliyowekwa kwa mujibu wa sheria.

10.4 POSTA

Chadema inatambua kuwa mfumo wa huduma za Posta ni muhimu katika kuwezesha mawasiliano na miamala ya kibiashara katika jamii iliyo na maarifa kwa kuimarisha soko la kimtandao pamoja na taasisi za kibiashara. Hii inajumuisha kuboresha upatikanaji wa huduma kwa kuzingatia mabadiliko katika soko

Chadema itaanzisha matumizi ya nambari za posta na mfumo wa anuani ya makaazi katika Mitaa ikiwa ni pamoja na kuboresha mfumo wa zamani uliokuwa unatumia “Sanduku la Posta” katika ofisi za Posta nchini.

Chadema itaanzisha huduma za posta ambazo zitasaidia biashara kwa mfumo wa mtandao na kuhakikisha bidhaa zinaagizwa kimtandao na kuwafikia watumiaji kwa urahisi. Chadema itahakikisha kuwa Serikali inamiliki mfumo wote wa Posta isipokuwa huduma mbalimbali zitakazokuwa zinatolewa zitaanyika kwa kushirikiana na sekta binafsi.

Kwa ujumla, Serikali ya Chadema itachukua hatua zifuatazo:

- a. Kuanzisha na Kuboresha Mfumo wa Anuani za Posta na Makaazi na kuziunganisha na mifumo ya kidigitali.
- b. Kupanua na Kuboresha Mfumo wa Kusafirisha Vifurushi kwa njia ya Posta
- c. Kuboresha Usimamizi wa Huduma za Posta
- d. Kugatua Mfumo wa Posta na Kuhakikisha Ushiriki wa Sekta Binafsi

11. MALIASILIA NA UTALII

Chadema inatambua hali halisi katika eneo hili na kupanga kuchukua hatua kuondoa mapungufu ya kiseru na kiutendaji katika enao hili. Chadema itatekeleza sera yake kuhusu maliasili ikiwa ni pamoja na:-

- a. Kusimamia uvunaji na matumizi ya rasilimali za Taifa kwa manufaa ya kila Mtanzania wa kizazi hiki na kijacho
- b. Kupiga vita ujangili na kuimarisha utunzaji wa hifadhi za taifa na mazingira
- c. Kutunza na Kuhifadhi Maeneo au Shughuli Maalum kwa ajili ya Utalii
- d. Kulinda hifadhi za wanyama, kutunza maliasili na urithi wa dunia kwa kizazi kijacho.
- e. Kusimamia utunzaji wa wanyamapori kama chanzo cha mapato kwa Serikali na ajira kwa wananchi.
- f. Kuhakikisha kuwepo kwa usimamizi endelevu wa wanyamapori utapelekea kupunguza migogoro katika hifadhi na kuboresha mahusiano mazuri kati ya mamlaka za hifadhi na jamii zinazonguka maeneo hayo.
- g. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba shughuli za hifadhi za Taifa zinasimamiwa vizuri ili kulinda hifadhi hizo bila kuathiri maisha ya wananchi wanaoishi jirani na hifadhi hizo.
- h. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba sehemu ya mapato yanayotokana na hifadhi za Taifa pamoja na shughuli za wanyama yanatumika kukabiliana na majanga pamoja na utunzaji wa mazingira kwa ajili ya manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.
- i. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itahakikisha kuwa inalinda, kuhifadhi na kuendeleza Bioanuai kwa ajili ya matumizi endelevu.

11.1 WANYAMAPORI

Chadema inachukulia usimamizi wa Wanyamapori kama hatua ya kutunza, kulinda na kuhifadhi wanyamapori na mimea asilia. Chadema inatambua kuwa maisha ya Wanyamapori yapo hatarini kutokana na mabadiliko ya tabia nchi, ujangili, kukata miti ovyo na shughuli nyingine za binadamu. Chadema inatambua kuwa wanyamapori wanatakiwa kulindwa kwa ajili ya kukuza utalii na biashara itokanayo na bidhaa za wanyamapori.

Chadema inatambua kuwa ipo mimea na wanyama ambao iko hatarini kupotea kutokana na majanga ya asili, magonjwa au shughuli za binadamu na kwamba kuna haja ya kutumia njia kadhaa ikiwemo kuwa na hifadhi maalum ya wanyamapori, kuzalisha mbegu nyingine, pamoja na kuwa na mkakati wa kuzuia kupotea kwa mimea husika .

Shughuli za maendeleo za binadamu dhidi ya maisha ya wanyamapori zisimamiwe ili kulinda hifadhi ya wanyama bila kupuuza maisha ya watu wanaoishi katika maeneo yanayozunguka mbuga za wanyama.

Serikali ya Chadema itaanzisha miradi ya elimu, kuhamasisha jamii na kushirikisha jamii kuhusu usimamizi wa wanyamapori hasa kwa jamii zinazopakana na mbuga za wanyamapori.

Serikali ya Chadema itahimiza matumizi endelevu ya wanyamapori kwa ajili shughuli za kijamii na kiuchumi. Mapato yote yanayotokana na sekta ya wanyamapori yatatumika pekee kwa ajili kutunza na kulinda wanyamapori na kulinda maeneo ya urithi wa dunia.

Pamoja na kuwa utalii ni moja wapo ya sekta zinazochangia kwa kiasi kikubwa katika pato la Taifa, bado maliasili zake hazijatumiwa vya kutosha ili kuongeza zaidi pato la Taifa, kutokana na mianya mingi kwa makampuni ya kitaalii ya ndani na nje kukwepa kodi ambayo ingepaswa kuingia katika mfumo wa Taifa.

Kutokana na changamoto mbalimbali zinazotokana na uwepo wa Wanyamapori, Serikali ya Chadema itarejea upya sera na sheria ya Wanyamapori ili kuendana na kasi ya ukuaji wa idadi ya watu na wanyama .

11.2 MISITU

Misitu ya asili na ambayo huchukua muda mrefu katika ukuaji wake kama mninga inapungua kwa kasi sana na karibu inatoweka kabisa katika ardhi ya Tanzania. Tatizo kubwa ni kuwa misitu hii inavunwa kiholela na uvunaji wake hauna tija kwa Taifa; mfano ni misitu iliyo mipakani mwa nchi jirani ambayo imekuwa ikivunwa na wageni wa nchi za jirani kwa kushirikiana na mamlaka za ndani katika maeneo husika. Na wakati haya yote yakitokea kasi ya upandaji wa miti mipya na hata miti kwa ajili ya uzalishaji wa nishati imekuwa ikisuasua na hivyo kuiweka nchi yetu katika hali hatarishi kugeuka kuwa jangwa.

Hakuna mipango mizuri na uvunaji endelevu wa misitu na utengenezwaji wa samani bora zaidi zitakazoweza kuuzwa nje.

Hata hivyo, Chadema kinatambua fursa zifuatazo katika eneo hili na kupanga kuchukua hatua kufanyia kazi fursa zifuatazo zilizo katika enao hili:

- a. Bado kuna maeneo makubwa yenye maliasili adimu ambayo yanaweza kutunzwa sasa kwa ajili ya vizazi vijavyo
- b. Maazimio na mikakati mbalimbali ya kuzuia uvunaji haramu wa maliasili za nchi.

Serikali ya Chadema itapitia upya sera ya misitu ili kuhakikisha kuwa misitu pamoja na mazao yake vinachangia katika kuongeza pato la taifa.

11.3 UHIFADHI WA UOTO WA ASILI NA MAENEO ASILIA

Chadema inaamini katika uhifadhi unaolinda uoto wa asili na maeneo asilia yakiwemo makazi ya asili ya binadamu.

Uoto wa asili ni muhimu kwa ajili ya maendeleo ya uchumi. Uhakika wa kuwa na chakula pamoja ugunduzi wa madawa mapya ya afya uko hatarini kwa sababu ya athari za kupotea kwa uoto wa asili. Bidhaa na huduma muhimu zinaathirika kutokana na hatari ya kupotea kwa uoto wa asili.

Sehemu ya hatua stahiki zitakazochukuliwa na serikali ya Chadema katika eneo hili ni:

- a. Kuchukua hatua za kurudisha na kuhuisha ikolojia ya maeneo oevu kwa ajili ya kulinda mazingira na viumbe vilivyopo.
- b. Kuhimiza uwepo wa miundombinu ambayo inalinda mazingira kwa kuanzisha maeneo maalum Mijini yanayohifadhi mazingira ya asili, maji na bustani za mimea ili kufanya jamii ione umuhimu wa kutunza mazingira.
- c. Kuweka mkazo katika kufanya tafiti za kulinda mbegu za wanyama na mimea ya asili iliyo hatarini kutoweka ili kulinda uoto wa asili na maeneo asilia.
- d. Kuhimiza uhifadhi wa misitu kwa ajili tafiti za afya na utalii.

Serikali ya Chadema itawahakikishia wananchi wa Tanzania kuwa wananufaika na urithi wa mali asili walizonazo kwa:

- a. Kusimamia utunzaji wa maeneo oevu utasaidia upatikanaji wa maji kwa ajili umwagiliaji, shughuli za kilimo endelevu na mabwawa ya samaki.
- b. Kuchukua hatua za kuchochea kuwepo na kuimarika kwa Utalii wa Mijini kwa kutenga maeneo yenye mazingira ya asili yenye mvuto wa kiutalii kwa lengo la kuongeza fursa za ajira

- c. Kusimamia kuwepo kwa hifadhi ya misitu yenye kusaidia katika uvumbuzi wa dawa mpya zitokanazo na mimea asilia na hivyo kuboresha sekta ya afya.

11.4 UTALII



Sekta ya utalii inaliingizia Taifa letu zaidi ya asilimia 25% ya mapato yake ya fedha za kigeni kwa taarifa zilizotolewa na Benki Kuu ya Tanzania (BOT). Sekta hii ndiyo inayotoa ajira rasmi nyingi baada ya sekta ya kilimo .

Serikali ya Chadema, itahimiza ushirikiano wa karibu kati ya sekta binafsi na sekta ya umma pamoja na kutekeleza mpango mahususi (rescue package plan) wa muda mfupi na muda wa kati wa kutenga fedha na vivutio vingine vya kikodi vyenye kulenga kushawishi na kuhimiza uwekezaji wenye lengo la kunusuru sekta hii na waajiriwa wake walioathiriwa na anguko la sasa la sekta hii.

Serikali ya Chadema, pamoja na sera zake za muda mrefu kuhusiana na sekta hii zinazoanishwa katika ilani hii, itakubali kubeba gharama za mkakati wa mawasiliano wenye kulenga kushawishi kurudi katika hali yake ya hapo awali kwa sekta hii ya utalii.

Serikali ya Chadema itatekeleza sera yake ya muda mrefu kuhusu utalii ikiwa ni pamoja na kuongeza Idadi ya Watalii Wanaokuja Nchini, kufungua vivutio vipya vya Utalii vilivyopo nchini na kuwa na Ulinzi wa Uhakika kwa Watalii

Katika kutekeleza hayo serikali ya Chadema itaazisha mchakato wa mashauriano na wadau kupata muafaka kuhusu maboresho ya sheria yatakayowezesha yafuatayo:

- a. Kuvutia Watalii wengi kutembelea nchini kwa njia ya matangazo ya kibiashara na kuhakikisha taarifa za maeneo asili yenye vivutio, tamaduni na maeneo ya kihistoria zinawafikia kwa wakati na ufasaha.
- b. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itaanzisha miundombinu ya utalii yenye viwango vya kimataifa kwa ajili ya kutoa huduma kwa Watalii kwenye maeneo ya bahari, maziwa, mito, misitu, wanyamapori, maeneo ya kihistoria, tamaduni na michezo.
- c. Serikali ya Chadema itaanzisha mfumo wa haki miliki katika filamu na picha zitakazopigwa katika maeneo yenye vivutio nchini.

Kwa ujumla serikali ya Chadema itaweka mkazo kiseru na kiutendaji ufuatiliwaji wa karibu yafuatayo:

- a. Kuchochea ujenzi wa miundombinu ya utalii nchini ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mahoteli na kuimarisha mafunzo



- b. Kuingia mikataba ya kimataifa kupitia Umoja wa Mataifa yakupambana na ujangili kwenye hifadhi, mbuga na masoko.
- c. Kuongeza idadi ya watalii nchini hadi kufikia milioni mbili kwa mwaka katika kipindi cha utekelezaji wa Ilani hii.

12. UZALISHAJI WA NISHATI NA MATUMIZI YA MADINI WENYE TIJA



12.1 Nishati

Chadema inatambua kwamba nishati ni nguzo muhimu katika kuboresha maisha ya watanzania na ujenzi wa taifa kiuchumi.

Kumekuwa na changamoto kubwa ya kupata nishati ambayo inaendana na ulinzi wa mazingira kutokana na chanzo kikuu cha nishati inayotumika nchini ni mkaa na ambao kwa kiasi kikubwa sio rafiki kwa mazingira.

Katika kukabiliana na changamoto hizi serikali ya Chadema itafanya yafuatayo;

- a. Serikali ya Chadema itaingia ubia na sekta binafsi katika kuzalisha, kusafirisha na kusambaza nishati ya umeme nchini
- b. Serikali ya Chadema itatumia madini kama dhamana katika kujenga miundombinu ya umeme nchini

- c. Mpango wa Serikali ya Chadema katika kuzalisha nishati ni:
- Uzalishaji wa Umeme wa maji
 - Umeme wa makaa ya mawe
 - Umeme wa nguvu za jua, upepo na biomas (Nishati Jadidifu)
 - Umeme wa gesi

Aidha Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi inaweka utaratibu wa kuzalisha, kusafirisha na kuuza Gesi kuleta mtaji

- d. Usambazaji wa umeme utazingatia uzalishaji na usafirishaji
- viwandani
 - reli na barabara, na
 - bandari
 - Majumbani na kwenye taasisi za umma na binafsi
- e. Kudhibiti rushwa za mikataba kwenye sekta ya Nishati kwa kuweka utaratibu wa wazi, uwajibikaji na kuhakikisha kuwa sheria zinafuatwa ikiwa ni pamoja na mikataba yote kulazimika kupitiwa na Bunge.

12.2 Madini

Chadema inatambua kwamba rasilimali za madini zilizopo Tanzania ni utajiri usioendelevu na urithi wa wote ndani ya vizazi vyote vya Tanzania. Hivyo hatuna budi kuitumia rasilimali hii kwa uangalifu ili vizazi vijavyo viweze kunufaika na rasilimali hii hata kama itakuwa imeshaisha.

Hivyo basi ili kuhakikisha kuwa madini yananufaisha kizazi cha sasa na kijacho, Serikali ya Chadema itachukua hatua zifuatazo;

- a. Kuhakikisha madini yanatumika kama dhamana ya mtaji kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mbalimbali kama vile maji, barabara, reli na nishati
- b. Uvunaji wa madini utakuwa maalumu kwa ajili ya mitaji ya; Nishati, hasa umeme na maji, Ujenzi wa viwanda , kujenga na kuboresha miundombinu ya uchukuzi
- c. Serikali ya Chadema itaweka utaratibu wa ubia katika uchimbaji wa madini baina ya raia na wageni kwa ajili ya kuwawezesha watazania ambao mitaji na teknolojia yao sio kubwa kuweza kunufaika kutokana na ubia na Makampuni ambayo yataingiza mitaji mikubwa na teknolojia ya kisasa katika uchimbaji wa Madini
- d. Serikali ya Chadema itaweka utaratibu wa kisheria juu ya misamaha ya kodi katika sekta hii ili kulipunguzia taifa hasara itokanayo na baadhi ya misamaha kwenye sekta hii
- e. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itaboresha sekta ya madini na kuwezesha wachimbaji wadogo kushiriki na kumiliki uchumi wa madini
- f. Serikali ya Chadema itapitia na kuboresha sheria za madini zilizopo ili ziendane na viwango vya kimataifa ili taifa liweze kunufaika na madini bila kuathiri uwekezaji

13. VIWANDA

Tangu kubinafsishwa kiholela kwa viwanda na mashirika ya umma nchini, taifa limeshuhudia ongezeko kubwa la uagizaji bidhaa toka nje ya nchi huku nyingi ya bidhaa hizo malighafi zake zikipatikana hapa nchini.

Aidha ubinafsishaji huo holela umesababisha viwanda vingi kufa na hivyo kuchangia ongezeko kubwa la ukosefu wa ajira kwa vijana nchini.

Ili kukabiliana na changamoto hii serikali ya Chadema itaanzisha viwanda vya kimkakati katika maeneo mbalimbali ya kisekta hususani kilimo, uvuvi na ufugaji ili kuyaongezea thamani mazao husika. Viwanda hivi vya kimkakati vitagusa matumizi anuwai ya rasilimali zetu kwa kutumia ubunifu, ugunduzi na teknolojia ya kisasa.

Ili kufikia hatua hii muhimu ya kukuza uchumi na pato la taifa, Serikali ya Chadema imelenga kufanya yafuatayo mara tu itakapo pata ridhaa ya kuongoza taifa;

- a. Kwa kushirikiana na sekta binafsi, Serikali ya Chadema itawezesha mchakato wa uanzishwaji wa Viwanda vikubwa vitatu vya kimkakati; kwanza, katika eneo la Liganga na Mchuchuma tutaanzisha kiwanda cha kisasa cha kuchakata, kufua na kuzalisha chuma. Pili, tutaanzisha Kiwanda Karagwe kwa ajili ya kuchakata bati (Tin) kwa ajili ya uzalishaji wa bidhaa za mabati. Tatu, tutaanzisha kiwanda cha kuchakata chuma kizito (Nickel) maeneo ya Kabanga na Ngasamo.
- b. Kwa kushirikiana na sekta binafsi, serikali ya Chadema itawezesha uanzishaji wa viwanda vikubwa vya kisasa vya kuchakata mazao ya misitu kwa ajili ya utengenezaji wa samani za maofisini na kuondoa kabisa uagizaji samani hizo kutoka nje ya nchi.

- c. Serikali ya Chadema itatenga bajeti ya kutosha kuwezesha utafiti wa kisanyansi na kiteknolojia, ubunifu na ugunduzi kwenye kiwanda cha Nyumbu kilicho chini ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania ili kiweze kuzalisha Magari ya kisasa, zana za kilimo, na zana nyinginezo za kivita kwa ajili ya matumizi ya nchi na kuuzwa nje ya Nchi.
- d. Serikali ya Chadema kwa kushirikina na sekta binafsi, itaanzisha kiwanda kikubwa cha madawa ya binadamu ili kuziba kabisa mwanya wa uhaba wa madawa katika ukanda wote wa Afrika Mashariki na Kati.
- e. Kwa kushirikiana na sekta binafsi, Serikali ya Chadema itaanzisha kiwanda kikubwa cha Karatasi na vifaa vingine vya maofisini ili kuondoa utegemezi wa uagizaji wa bidhaa hizi nje ya nchi
- f. Kwa kushirikiana na sekta binafsi, serikali itawezesha uanzishwaji wa kiwanda kikubwa cha bidhaa zitokanazo na pamba, ili kuongeza soko la pamba kwa kuuza nyuzi badala pamba ghafi
- g. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi, itaweka mazingira rafiki ya kuanzishwa kwa Viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo na uvuvi
- h. Kwa kushirikiana na sekta binafsi serikali ya Chadema itawezesha mchakato wa kuanzishwa kwa kiwanda kikubwa cha kuchakata madini ya kimkakati (strategic rare earth metals) ili kuwezesha kuanzishwa kwa uundaji na utengenezaji wa Vifaa vya kielektroniki
- i. Kwa kushirikiana na sekta binafsi Serikali ya Chadema itaanzisha kiwanda kikubwa cha kuchakata na kuongeza thamani ya zao la korosho.

14. MICHEZO, SANAA NA UTAMADUNI

Chadema inaamini kwamba michezo, utamaduni na sanaa ni utambulisho wa Taifa letu kitaifa na kimataifa, aidha tunaamini kuwa michezo mbali ya kuwa ni burudani, ni uchumi na chanzo kikuu cha ajira.

Serikali iliyopo madarakani haijawekeza vya kutosha katika kuboresha michezo nchini ikiwemo kutenga bajeti kidogo katika sekta ya michezo, sanaa na utamaduni.

Kutokuwa na mkakati wa kuinua michezo na utamaduni nchini kumesababisha timu mbalimbali za Taifa kutofanya vizuri katika mashindano mbalimbali ya kimataifa.

Aidha kushindwa kuwa na mikakati ya kukuza utamaduni na Sanaa nchini kumewafanya wasanii kutokua na uhakika wa kipato na kuwatumia wakati wa kampeni pekee na baadae kuwaacha wakihangaika bila kuwepo mpango madhubuti wa kuinua kazi za sanaa na utamaduni.

Serikali imeshindwa kuwekeza kwenye viwanja vya michezo vyenye hadhi kimataifa ambapo nchi inakosa mapato kwa kushindwa kuendesha mashindano ya kimataifa hapa nchini.

Chama cha Mapinduzi kilipoka viwanja vya michezo ambavyo vilikuwepo wakati wa Chama kimoja na kujimilikisha huku kikifahamu kwamba wananchi wote bila kujali itikadi zao walichangia nguvu na fedha kujenga viwanja hivyo.

Aidha, Serikali imeshindwa kuboresha Chuo cha Sanaa pamoja na kushindwa kuwalea wasanii wa muziki, filamu, sarakasi na aina zingine za sanaa jambo linalopelekea Baraza la Sanaa (**BASATA**) kuwa Msimamizi na kuwaadhibu wasanii badala ya kuwa na mkakati wa kuboresha na kutangaza utamaduni wetu kimataifa ili kuwapatia wasanii kipato.

Serikali ya Chadema itafanya mambo yafuatayo;

- a. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba mitaala ya michezo, sanaa na utamaduni inarejeshwa na kuboreshwa kuanzia Shule za Msingi.
- b. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba timu zote zinazocheza ligi mbalimbali za mpira wa miguu nchini ikiwemo ligi kuu zinakua na shule za michezo (sports academy) kwa ajili ya Watoto bila kuathiri mfumo na utaratibu wa kupata masomo mengine katika mfumo wa elimu.
- c. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba inarudisha kimbakati na kibajeti utaratibu wa mashindano ya UMITASHUMTA kwa shule za Msingi, UMISETA kwa Shule za Sekondari pamoja na mashindano ya Vyuo vyote kwa ajili kutambua vipaji mbalimbali miongoni mwa wanafunzi na kuhakikisha mashindano hayo yanakuwa na tija ya kuendeleza Taifa letu kimichezo na kiutamaduni kuliko ilivyo sasa.
- d. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itahakikisha kwamba kwa kushirikiana na sekta binafsi kila mwaka inatengwa bajeti kwa ajili ya ujenzi wa viwanja vyenye hadhi ya kimataifa kwa ajili ya kuendesha ligi za kimataifa na kuboresha hadhi ya ligi ya ndani
- e. Serikali ya Chadema itahuisha utendaji na uwajibikaji wa Shirikisho la Mpira la Tanzania na Zanzibar ili watekeleze majukumu yao kitaalam pamoja na kuwa na Bajeti inayotosheleza mahitaji ya maendeleo ya mpira nchini ikiwemo usimamizi imara wa ligi kuu
- f. Serikali ya Chadema itahuisha Taasisi ya Sanaa ya Bagamoyo (TASUBA) na kuifanya kuwa Chuo Kikuu cha Sanaa nchini pamoja na kuhakikisha kwamba kila Mkoa unaanzisha

- angalau chuo kimoja kwa ajili ya Sanaa na kuwa na hadhi ya kutoa cheti na Diploma.
- g. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba inahusha kodi kwenye kazi za sanaa kwa wasanii wa ndani ili kuhakikisha kwamba wasanii wananufaika na jasho lao.
 - h. Serikali ya Chadema itahakikisha inakua na mkakati wa kuwa karibu na makampuni makubwa ya mitandao ambayo inahusha na uuzaji wa kazi za sanaa (Mfano **YouTube**) duniani ili kuhakikisha kwamba kazi za Wasanii zinafanywa kwa kukidhi viwango vya makampuni hayo ili kuongeza kipato cha Wasanii na kuwatangaza duniani.
 - i. Serikali ya Chadema itaweka mpango wa muda mfupi wa kufanya maboresho ya michezo na sanaa nchini kuwa sehemu ya kipato na kuhakikisha tunawezeza kukuza wasanii na wanamichezo kimataifa kuliko ilivyo sasa ambapo Serikali hushabikia mafanikio ya Wanamichezo na Wasanii ambao wamepiga hatua kwa juhudi binafsi bila msukumo na uwezesaji wa serikali.
 - j. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba inapanua wigo wa kazi za Tume ya Sayansi na Utafiti kulea vipaji na ugunduzi ikiwemo vipaji katika michezo, sanaa na utamaduni.
 - k. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itaanzisha mashindano yatakayowahusha Watu wenye ulemavu ili kuonyesha vipaji vyao na kuwafanya kunufaika na vipaji vyao nchini na kuwafanya washiriki kwenye mashindano kama hayo kimataifa.
 - l. Serikali ya Chadema kwa kushirikiana na sekta binafsi itaanzisha mchakato wa kujenga jengo kubwa la sanaa za maigizo na maonyesho (Arena) kwa ajili ya kukuza vipaji vya wasanii

15. ULINZI NA USALAMA

Ulinzi na Usalama ni eneo muhimu katika ustawi na uwepo wa Taifa letu. Chadema inaamini kwamba ulinzi na usalama ni kazi ya msingi na muhimu kwa serikali kwa ajili ya kulinda Watu, mali zao pamoja na kuhakikisha kuwa mipaka ya nchi ipo salama.

Pamoja na kutambua baadhi ya kazi nzuri zinazofanywa na vyombo vya ulinzi na usalama bado zipo changamoto nyingi zinazokabili vyombo hivi na hivyo kupelekea kushindwa kufanya kazi zao kwa ufanisi.

Vipo viashiria kadhaa vilivyojitokeza katika utendaji wa Serikali ya awamu ya tano ambapo kama nchi tumeshuhudia baadhi ya wananchi wakiuawa, kutekwa, kuteswa, kupigwa risasi, kuharibiwa biashara zao kinyume na sheria, kufukuzwa kazi bila kuzingatia taratibu za kisheria jambo ambalo linazua malalamiko na manung'uniko miongoni mwa wananchi na hivyo kupelekea kuathiri ulinzi na usalama wa nchini.

Wananchi wanaoishi mipakani bado wameendelea kusumbuliwa na vyombo vya dola kuhusu uraia wao jambo linalotengeneza hisia miongoni mwao kwamba sio raia wa nchi hii kwa sababu ya kuzaliwa mipakani. Chadema inatambua kwamba zipo changamoto ya baadhi ya wahalifu kutoka nchi jirani kuingia nchini na kufanya matukio ya kihalifu ikiwa ni pamoja na kuingia kwa jinai kwenye sehemu ya ardhi ya nchi yetu kinyume na mipaka iliyopo kwa mujibu wa sheria za kimataifa.

Serikali ya Chadema itafanya mambo yafuatayo ili kuboresha masuala ya ulinzi na usalama;

- a. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba vyombo vyote vya Ulinzi na usalama vinapata bajeti yake kwa ukamilifu kama ilivyopitishwa na Bunge na hivyo kuondoa na kupunguza changamoto ya vifaa, makazi na sare za vyombo hivyo.

- b. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba vyuo vya mafunzo vinavyotumiwa na vyombo hivyo vinaboreshwa pamoja na kuhakikisha uwepo wa miundombinu na mazingira mazuri ya kujifunzia.
- c. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba mishahara pamoja na marupurupu mengine inaboreshwa na hivyo kuwafanya Askari kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.
- d. Serikali ya Chadema itaanzisha bima maalum ya afya kwa vyombo vya Ulinzi na Usalama wawapo kazini na baada ya kustaafu vikiwemo Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), Polisi, Magereza, Uhamiaji na Zima moto na Uokoaji.
- e. Serikali ya Chadema itarudisha na kuboresha utaratibu wa kutoa kodi kwenye maduka (dutyfree shops) ya Vyombo vya Ulinzi na Usalama ili kutoa motisha kwa Askari wakati utekelezaji wa majukumu yao na pia watakapostaafu kuendelea kutumia maduka hayo.
- f. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba Jeshi la Magereza linahamishiwa Wizara ya Katiba na Sheria ili kuleta uhusiano mzuri wa utekelezaji wa majukumu yao.
- g. Serikali ya Chadema itaweka utaratibu mpya kisheria ili Jeshi la Uokoaji na Zimamoto lihamishiwe kiutendaji katika ngazi ya Halmashauri ili kuwa karibu na wananchi isipokua masuala ya kisera na utendaji wa jumla utatolewa na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji katika ngazi ya Taifa kwa utaratibu utakaowekwa
- h. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba utendaji wa vyombo vya Ulinzi na Usalama unazingatia ustawi na uwepo usalama kwa wananchi na mali zao
- i. Serikali ya Chadema itahuisha utaratibu uliopo sasa wa utoaji wa pasi za kusafiria ili ziweze kutolewa kwenye ngazi ya

- Kanda na Mikoa na hivyo kuwa na ufanisi. Aidha, mipaka ya nchi itaboreshwa ili vituo vyote vya Uhamiaji, vyombo vya Ulinzi na Usalama na ofisi za Mamlaka ya Mapato mipakani kufanya kazi kwa saa 24 kwa ajili ya kuboresha ufanisi wa maeneo hayo.
- j. Serikali ya Chadema itahakikisha kwamba inaajiri Askari wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama wa kutosha wenye mafunzo na weledi kwa ajili ya kuboresha uwiano kati ya Askari na idadi ya wananchi nchini.
 - k. Serikali ya Chadema itahuisha utaratibu wa Vijana kupata mafunzo ya Jeshi la Kujenga Taifa yakiambatana na mafunzo ya ufundi ili kuwajenga kiuwezo na kimkakati kwa ajili ya Ulinzi na Usalama wa nchi.
 - l. Serikali ya Chadema itazifanyia marekebisho makubwa sheria mbalimbali zinazounda vyombo vya Ulinzi na Usalama ili kuendana na mahitaji ya kijamii pamoja na maendeleo ya kiteknolojia duniani ili kulifanya Jeshi kuwa kitovu cha kiteknolojia bora na ya kisasa kwa sekta zote za uzalishaji na utoaji wa huduma.

16. TANZANIA KATIKA DIPLOMASIA YA KIMATAIFA

Tanzania ilikuwa inajulikana duniani kwa misimamo ya kimantiki na katika kuendesha na kuunga mkono harakati za ukombozi wa wanyonge popote duniani.

Serikali imepoteza dira na mwelekeo katika ulimwengu wa kidiplomasia na haijaweza kujenga mahusiano baina yake na washirika wake wa tangu enzi za kupambana na Mkoloni, zaidi ni kuwa sasa imepoteza heshima iliyokuwa imejijengea kimataifa katika diplomasia.

16.1 KUKUZA NAFASI YA TANZANIA KATIKA DIPLOMASIA YA KIMATAIFA

Lengo la Chadema kuhusu ushirikiano wa kimataifa ni kuhuisha nafasi ya Tanzania katika jumuiya za kimataifa ili kushiriki kukomesha uonevu, ukandamizaji na kuchochea utawala bora na ukuaji wa demokrasia, hasa katika nchi za kiafrika. Katika kufikia lengo hilo serikali ya Chadema itafanya mambo yafuatayo;

- a. Serikali ya Chadema itajenga mahusiano na nchi mbalimbali duniani kwa kuzingatia diplomasia ya uchumi inayolenga kubadilisha na kukuza uchumi wa Taifa. Serikali ya Chadema itajenga ushirika na nchi rafiki kwa kuzingatia mashirikiano pasipo kunyonyana.
- b. Katika kutimiza azma ya kujiendeleza katika sekta ya sayansi na teknolojia, Serikali ya Chadema itaweka mkazo katika kuimarisha mahusiano yanayolenga kuiwezesha Tanzania kuiga na kuchota maendeleo ya kiteknolojia yaliyofikiwa katika nchi za Asia na hasa China.
- c. Serikali ya Chadema itahuisha juhudi za Tanzania za kuhakikisha kuwa bara la Afrika linaungana kijamii, kiuchumi na kisiasa kama walivyoazimia waasisi wa bara

hili, Mwalimu Nyerere na Kwame Nkrumah.

- d. Serikali ya Chadema itabuni na kusimamia mikakati ya kuiweka Tanzania kuwa kiongozi katika kuhitimisha lengo la kufikia Shirikisho la Afrika Mashariki
- e. Serikali ya Chadema itashiriki vikao muhimu vya Kimataifa kama vile Mkutano Mkuu wa Umoja wa Mataifa, Vikao vikuu vya Umoja wa Afrika na vinginevyo
- f. Serikali ya Chadema itafuta sheria zote ambazo sio rafiki kwa uwekezaji na wawekezaji kutoka mataifa mbalimbali

16.2 IDARA YA UHAMIAJI

Kumekuwa na changamoto kubwa miongoni mwa wananchi kuhusu upatikanaji wa hati za kusafiria, kupata vyeti vya kuzaliwa na kupata vitambulisho vya taifa.

Kwa sasa Idara ya uhamiaji ina jukumu la kuandikisha watanzania na wageni wote nchini, Wakala wa usajili wa vizazi na vifo wanawajibu wa kutoa vyeti vya kuzaliwa na vifo huku Mamlaka ya vitambulisho vya taifa ikiwa na jukumu la kutoa vitambulisho vya uraia .

Ili kukabiliana na changamoto hizo serikali ya Chadema itafanya mambo yafuatayo;

- a. Serikali ya Chadema itaunganisha wakala wa usajili wa vizazi na vifo (RITA), mamlaka ya vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Idara ya Uhamiaji kuwa chombo kimoja .
- b. Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa watoto wote watapewa hati ya kuzaliwa ikionyesha uraia wao kwa mujibu wa sheria na baada ya kufikisha umri wa miaka 18, watapewa vitambulisho vya kitaifa ambavyo vitakuwa vimeunganishwa kwenye mtandao mmoja mkubwa wa kitaifa. Vitambulisho hivi vitatumika pia kutunza kumbukumbu muhimu za taarifa zao (electronic biometric regiter).

- c. Serikali ya Chadema itaweka utaratibu kwa wageni wote waingiao nchini watatakiwa kutumia hati zao za kusafiria kama vitambulisho vyao, isipokuwa wale tu watakaopewa vibali vya kufanya kazi watatengenezewa vitambulisho vya kitaifa vikionyesha pia uraia wao.
- d. Serikali ya Chadema itapunguza urasimu na ukiritimba katika upatikanaji wa hati za kusafiria kwenda nje ya nchi ili kuhakikisha kuwa huduma hii inapatikana katika kila mkoa kwa wakati. Hata hivyo, Hati ya kusafiria ni haki ya kila mwananchi anayeomba.
- e. Kwa kuwa kutakuwa na mtandao wa kitaifa wa orodha ya raia wote na kumbukumbu zao za makosa mbalimbali, serikali ya Chadema itaweka utaratibu wa kuhakikisha kuwa Mikoa inakuwa na jukumu la kushughulikia maombi ya hati za kusafiria kwa kushirikiana na idara ya Uhamiaji Makao Makuu ambayo itakuwa na jukumu la kuchapa na kusambaza hati hizi. Ili kuhakikisha kuna ufanisi na tija, serikali ya Chadema itahakikisha kuwa maombi yote ya hati za kusafiria yatakuwa yamefanyiwa kazi ndani ya siku zisizozidi ishirini na moja (21).
- f. Serikali ya Chadema itapitisha mabadiliko ya Katiba yatakayoruhusu kuwa na uraia wa nchi zaidi ya moja. Hivyo, Serikali ya Chadema itahakikisha kuwa hakuna Mtanzania yeyote ambaye anavuliwa Utanzania wake kwa vile amechukua uraia wa nchi nyingine. Hii ina maana kuwa Tanzania itaendelea kumtambua Mtanzania hata kama amepata uraia wa nchi nyingine isipokuwa kama tu mtu huyo atakuwa ameukana uraia wa Tanzania yeye mwenyewe.
- g. Serikali ya Chadema itaanzisha idara maalum ya kusimamia Raia wa Tanzania walio Nje ya Nchi ambao watatambulika kuwa ni wananchi wote wa Tanzania pamoja na uzao wao. Watoto watakozaliwa au ambao wamezaliwa na Watanzania nje ya nchi na wamefikisha umri wa miaka 18 wataweza kuomba pasi za kusafiria za Tanzania.

- h. Serikali ya Chadema itaanzisha utaratibu wa kuwatumia Watanzania walio nje ya nchi katika kutoa mchango wa ujenzi wa taifa kwa utaratibu ambao utawekwa. Lengo ni kuweza kuchota na kutumia ujuzi na utaalamu mbalimbali uliopo baina ya wananchi hao.
- i. Serikali ya Chadema itaweka utaratibu kwa watoto watakozaliwa na mzazi mmojawapo akiwa ni mtanzania, mtoto husika ataendelea kutambulika kuwa ni raia hadi hapo atakapoamua mwenyewe kuukana uraia wa Tanzania baada ya kufikisha umri wa miaka 18 .

